**29 AGOSTI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 29 Agosti, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA**

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama sote tunavyojua mara baada tu ya kuahirisha Mkutano wa Kumi na Moja, Bunge letu lilipata msiba wa kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mtega alifariki tarehe 1 Julai, 2023 kwa ajali ya kugongwa na trekta *(power tiller)* shambani kwake Chimala - Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya. Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliagwa katika uwanja wa Chimala, Wilaya ya Mbarali siku ya tarehe 4 Julai, 2023 na hatimaye kuzikwa tarehe 5 Julai, 2023 katika Kijiji cha Lugalawa, Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima ya mpendwa wetu naomba tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka mwenzetu na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzishe kwa amani.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka Marehemu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega)*

**SPIKA:** Bwana ametoa, Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa nyingine, kwanza ni kuhusu Kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Bunge ya Kanuni ilifanya kikao tarehe 24 Agosti, 2023, ajenda kuu ya kikao hicho ilikuwa ni kufanya marekebisho katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Marekebisho yaliyohitaji kufanyika yanatokana na changamoto zilizojitokeza katika utendaji kazi wa Kamati, kufuatia marekebisho yalifanyika mwezi Februari, 2023 na marekebisho ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais mwezi Julai, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati iliridhia kufanya marekebisho katika kifungu cha sita kinachoainisha Kamati na Wizara inazozisimamia na kifungu cha tisa kinachobainisha majukumu ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo sasa itaendelea kusimamia shughuli za Wizara Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi;

(b) Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria imeongezewa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji;

(c) Kamati ya Maji na Mazingira itasimamia shughuli za Wizara ya Maji na masuala ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira;

(d) Kamati ya Bajeti itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha, Tume ya Taifa ya Mipango pamoja na shughuli nyingine kama zilivyoorodheshwa katika kifungu cha tisa cha Nyongeza ya Nane.

Waheshimiwa Wabunge, marekebisho hayo yamewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua za kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Nyongeza ya Nane Mpya itaanza kutumika rasmi mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Hakutakuwa na Toleo jipya la Kanuni, hivyo Toleo la Februari, 2023 litaendelea kutumika isipokuwa kwa Nyongeza ya Nane ambapo ile iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali ndiyo itakayotumika.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa nyingine ya Spika inazungumzia Miswada ambayo Bunge hili liliifanyia kazi. Katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Bunge lilipitisha miswada saba ya sheria kama ifuatavyo: -

(i) Kwanza, Muswada wa Sheria ya Tume ya Mipango wa mwaka 2023;

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa wa mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service Amendment Bill, 2023);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho yaliyotokana na Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa mwaka 2023 *(The Laws Revision (Miscellaneous Amendment) Bill, 2023);*

(iv) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2023 *(The Public Private Partnership Amendment Bill, 2023);*

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2023);*

(vi) Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha wa mwaka 2023 *(The Appropriation Bill, 2023);* na

(vii) Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2023 *(The Finance Bill 2023)*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili tukufu kuwa tayari miswada hiyo saba imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwa sheria za nchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa zimekuwa sheria za nchi na zina majina yafuatayo: -

(i) Sheria ya Tume ya Mipango (Na. 1) ya mwaka 2023;

(ii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa (Na. 2) ya mwaka 2023 *(The Tanzania Intelligence and Security Service Amendment Act (No. 2) of 2023);*

(iii) Sheria ya Marekebisho yaliyotokana na Urekebu wa Sheria Mbalimbali (Na. 3) ya mwaka 2023 *(The Laws Revision Miscellaneous Amendment Act (No. 3) of 2023);*

(iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Na. 4) ya mwaka 2023 *(The Public Private Partnership Amendment Act (No. 4) of 2023);*

(v) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) ya mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (Act No. 5) of 2023);*

(vi) Sheria ya Matumizi ya Fedha (Na. 6) ya mwaka 2023 *(The Appropriation Act (No. 6) of 2023);* na

(vii) Sheria ya Fedha (Na. 7) ya mwaka 2023 *(The Finance Act (No. 7) of 2023)*.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo ilikuwa Taarifa ya Spika na sasa tutaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hati za Kuwasilisha Mezani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Feleshi.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, (No. 2) of 2023)*.

**SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) ya Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, (No. 2) of 2023)*.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali.

Ofisi ya Waziri Mkuu, tutaanza na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 1

**Malalamiko ya wastaafu dhidi ya kikokotoo**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kuhusu malalamiko ya wastaafu juu ya kikokotoo kinachotumika kupiga mahesabu na kulipa mafao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitangaza matumizi ya kanuni mpya ya mafao (kikokotoo) ya pensheni kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 kupitia Gazeti la Serikali Na. 357 Toleo la tarehe 20 Mei, 2022. Kanuni hiyo iliandaliwa kwa kuzingatia haja ya kuboresha na kuwianisha mafao ya wanachama na kuifanya Mifuko ya Pensheni kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuwaelimisha wananchi hususani waajiri na wanachama wa Mifuko ya Pensheni wakiwemo wastaafu kuhusu faida ya kanuni mpya ya mafao ya pensheni. Hivyo, Serikali kupitia Mifuko ya

Pensheni na kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)* imejipanga na inaendelea kutoa elimu ya Kanuni hiyo. Hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2023, Mifuko iliweza kutoa elimu kwa jumla ya waajiri 5,580 kati ya waajiri 6,200 waliopangwa kufikiwa kipindi hicho. Aidha, wanachama 131,497 walifikiwa na mafunzo hayo. Mifuko itaendelea kutoa elimu kama sehemu ya majukumu yao ya kila siku, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusiana na kikokotoo hicho na inaelekea hakuna mpango wa kukirekebisha.

Je, Serikali imejipangaje hata hicho kiasi ambacho kinatolewa, kitolewe kwa wakati?

Swali la pili, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wastaafu sasa hasa wale wanaopata kiasi cha chini, mathalani shilingi 100,000 kwa mwezi, wanaongezewa kiwango hicho cha chini cha pensheni kwa kadri ambavyo mishahara inavyoongezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Priscus Tarimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosisitiza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba, ndiyo maana tunaendelea kutoa elimu. Suala la kwamba kuna malalamiko, wanufaika wa mifuko hii ya pensheni, katika utoaji wa fedha kulikuwa kuna changamoto ya uwiano wa utoaji wa mafao, pia kulikuwa na changamoto ya uendelevu wa mifuko, tulikuwa na changamoto pia ya mkupuo wa malipo, kwa sasa katika mkupuo wa malipo

wanufaika ni asilimia 81 ya wanachama wote, asilimia 19 mafao yao ya kila mwezi yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa katika mkupuo wa malipo, wanufaika ni asilimia 81 ya wanachama wote, na asilimia 19% mafao yao ya kila mwezi yameongezeka. Pia katika kipindi hicho utaweza kuona kwamba katika malipo yale ya kila mwezi, ilikuwa wanaweza kulipwa kwa asilimia 50, lakini sasa yamefikia asilimia 67 ya malipo. Hayo ni maboresho ambayo yametokana na utafiti uliofanyika. Tulifanya *actuarial valuation,* kwa kuwa mifuko hii ilikuwa na hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka tulikuwa tuna mifuko mingi ya *GPF*, *PSPF*, *LAPF* na *NSSF*. Mifuko hii kwa ujumla ilikuwa inashindana kwa wanachama wale wale. Utaratibu na maamuzi ya kuiweka pamoja mifuko hii imeleta tija kubwa na sasa mifuko imetoka *from loss making trend to profit making venture*. Kwa sehemu kubwa utaweza kuona, katika utaratibu huu, ndiyo maana tunaendelea kutoa elimu kwa sababu faida ni nyingi kuliko hasara ambazo zilikuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tutaendelea kutoa elimu. Mheshimiwa Mbunge kama anadhani kuna watu wanalalamika, wote ambao wamekuwa wakifika kwa kutokuelewa utaratibu huu ofisini, wamekuwa wakipewa elimu na wameona faida hii. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama anao watu hao, nitashirikiana naye katika kutoa elimu kama jinsi ambavyo mifuko imeendelea kutoa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wako watumishi wa Serikali wakiwemo walimu ambao walikumbwa na mfumo huo wa kikokotoo wa muda katika kile kipindi ambacho kilianza kutumika, lakini mpaka sasa walimu hao mfumo wao wa pensheni haueleweki na hauko sawa: Nini kauli ya Serikali kuhusiana na walimu hao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama alivyouliza kwamba mifumo ya ulipaji wa mafao ya walimu haueleweki.

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu uliofanyika wa kuunganisha mifuko na kutengeneza uwiano sawa wa malipo haukuacha kundi lolote nje likiwemo kundi la walimu. Kwa hiyo, kama kuna sehemu ambayo anadhani kwamba kuna walimu wana changamoto hiyo, mimi nilipokee tu jambo hili kutoka kwake na nikalifanyie kazi, kwa sababu mfuko huu haujabagua kundi lolote katika kutengeneza maslahi ya wafanyakazi wetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika jibu ambalo Mheshimiwa Waziri ametoa, amesema wanufaika kwa sasa hivi wameongezewa pesa kwenye yale mafao ya kila mwezi, lakini lalamiko lao kubwa ni mafao ya mkupuo ambayo mmetoa asilimia 50 mpaka 30. Leo mtu anayestaafu ambaye angepaswa kulipwa shilingi milioni 100, anapata milioni 50. Huo ndiyo msingi wa swali: Ni lini mtaleta sheria mbadilishe ili wastaafu wapate asilimia 50 waweze kujikimu ili sasa wakipata hicho cha mwezi, tayari msingi utakuwa una maana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nazidi kusisitiza kwamba suala hili ni la uelewa tu na elimu ambayo tutaendelea kuitoa. Mafao katika hatua ya awali katika Mifuko hii ya *GEPF*, *PSPF*, *LAPF* pamoja na *PPF* na *NSSF,* kila mfuko ulikuwa na aina yake ya utoaji wa mafao kulingana mfuko. Pia kwa hatua ya sasa, ukiangalia kwenye hili suala analosema la malipo ya Mkupuo, yalikuwa asilimia 25 na kwa mapenzi ya dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kupitia vikao, mashirikisho ya vyama vya wafanyakazi sasa

hivi imefikia asilimia 33 ya ulipaji wa mafao hayo, hayakufika kwenye hiyo asilimia 50 ambayo anaisema kwenye hatua ya awali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili tutaendelea kutoa elimu bila kuchoka, na wanufaika ambao ni wanachama wenyewe hawajawa na tatizo kubwa hili. Kama wapo, nazidi kusisitiza kwamba Serikali tuko tayari kuwasikiliza na kuwahudumia ili kuweza kuhakikisha manufaa hayo wanayapata. Serikali hii inawapenda sana wastaafu na ndiyo maana maboresho yamefanyika kila wakati; kisera, kisheria, kimiundo, kimfumo na utoaji. Hata kwenye utoaji sasa tumeenda katika teknolojia ya tehama, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona mmesimama. Niwakumbushe tu, maswali yaulizwe kwa kifupi ili kutoa nafasi kwa Wabunge wengi kuuliza maswali. Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kikokotoo ni kwa ajili ya watumishi na wastaafu; na uhalisia ni kwamba watumishi na wastaafu hawakitaki kikokotoo hiki: Ni lini Serikali italeta Muswada hapa wa kufuta kikokotoo hiki ili kuondoa kero kwa watumishi na wastaafu ambao hawakitaki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, *no research no right to speak*. Katika uhalisia wa *actuarial report* na utafiti uliofanyika, unufaikaji wa wanachama ni asilimia 81 ya wanachama wote, na asilimia 19, nadhani kama mtu atakuwa na hoja na hakubaliani, naye afanye utafiti na atuambie. Sisi tutaendelea kutoa elimu. Kwa kufanya hivyo, kwa sababu inaonekana suala linaanzia pengine kutokuwa na picha ya pamoja, tutaona umuhimu wa kuweka semina kwa ajili ya Wabunge ili kuweza kupata uelewa wa pamoja na kuwasaidia vizuri wanachama wetu kuliko kuwapotosha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa watumishi waliolipwa mafao pungufu hasa walimu; na wanapofuatilia wanaambiwa walipe gharama kwa ajili ya ufuatiliaji Dodoma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Nyoka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa wastaafu ambao michango yao haikupelekwa, kwanza ni kosa kisheria, kwa sababu sheria zetu zinamtaka mwajiri kuwasilisha michango ya mwanachama kila mwezi, lakini pia kama kuna changamoto za hao wastaafu ambao wanaambiwa tena pia waanze kupeleka michango yao wenyewe, hilo naomba nilichukue na ni jambo *serious* nahitaji nilifanyie kazi siku ya leo, nikitoka hapa niongee na Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya hatua zaidi.

**SPIKA:** Inaoneka kila Mbunge ana wastaafu kwenye eneo lake. Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza: Ni lini Serikali itamaliza kabisa malalamiko ya wastaafu wa zamani wakiwemo wale wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa umemsikia sehemu ya mwisho, anasema wakiwemo wale wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Masuala yote ya wastaafu tumeendelea sana kuboresha katika kuwasikiliza na pia kutatua changamoto zao. Hili suala la wastaafu wa Afrika Mashariki lilikuwa ni suala la kimahakama na Mheshimiwa kama unavyofahamu maamuzi ya Mahakama ndiyo huzingatiwa. Kwa hiyo, tutaangalia, wapo wengine ambao walikuwa kwenye hatua ya kufanya *execution of decree* ambayo ilitolewa na Mahakama na kulikuwa kuna

hatua mbalimbali za kwenda kudai mafao hayo kwa waajiri. Kwa hiyo, liko katika utaratibu wa usukumwaji na ufuatiliaji kwa mfumo wa kimahakama, lakini kwa yale ambayo yamekuja upande wetu, tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kama kuna *issue substantial* na *specific* kwa wastaafu kwenye eneo na jimbo lako, nitapenda nizipate ili tuzifanyie kazi. Kwa wote waliowahi kuleta, tumezifanyia kazi. Kwa hiyo, nawaomba sana, badala ya kusubiri, basi tutumie fursa hii kuweza kufanya hiyo kazi na kwenye semina ambayo tutaitoa tena kwa mara ya pili, itatusaidia sana kuweza kupata picha ya pamoja na kutatua changamoto hizi, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona lakini ni dhahiri Mheshimiwa Naibu Waziri ameshajibu maswali mengi kwenye eneo hili. Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshaonesha utayari, kama Mbunge anayo changamoto ya wale wanaoleta, ukiacha yale ya jumla tunayoyasema, apelekewe. Kwa kweli mimi ni shahidi, anafanya kazi nzuri yeye pamoja na Mheshimiwa Waziri, wanasikiliza. Yaani ukiwapelekea hoja, inafuatiliwa na ama mtumishi au mstaafu wako anasaidiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tupeleke hizo hoja mahususi, lakini zile za jumla, nadhani hoja yako Mheshimiwa Naibu Waziri ya kuendelea kutoa mafunzo ni ya muhimu. Kwa sababu Hifadhi ya Jamii lazima ijulikane kwamba ni hifadhi ya jamii. Ikionekana kwamba Hifadhi ya Jamii ni kwa ajili ya pesa ya uwekezaji ukistaafu, inaleta kidogo changamoto hapo. Kwa hiyo, ni kuelimisha jamii ili wajue nini wanapaswa kufanya na hizo pesa zinazotunzwa ni kwa ajili ya nini?

Nami nawapongeza, kwa sababu tulishasema kuhusu vile viambatisho mnavyoviomba kwa wastaafu, mmepiga hatua kubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza na mwendelee kufanya hivyo ili wastaafu wasiendelee kuteseka kupata mafao yao.

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Ni dhamira ya Rais wakati wote kuweza kuwahudumia vizuri wastaafu hawa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Kumaliza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kizazi – Kibondo**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Kizazi – Kibondo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, karibu tena Bungeni. Tumefurahi kukuona. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni siku yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa takribani miezi mitatu tangu nipate changamoto za kiafya, naomba kwa dhati ya moyo wangu nitoe shukrani zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyenijalia uhai, afya njema na kuniwezesha kurejea kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kulijenga Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa dhati ya moyo wangu, nitumie fursa hii ya Bunge tukufu kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameniwezesha kwa upendo wake na wema wake kwangu na Watanzania wote na kuniwezesha kupata

matibabu na hatimaye kurejea kuendelea kulijenga Taifa letu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunamwombea sisi Watanzania aendelee kuwa na afya njema aendelee kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, nawashukuru sana Viongozi Wakuu wa Serikali, nikianza na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninamshukuru sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru sana kwa ushirikiano wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe mwenyewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa viwango mwenye upendo. Ninakushukuru sana sana kwa ushirikiano wako na Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Bosi wangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, alikuwa nami muda wote na katika kila hatua ya matibabu yangu; na pia Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Deo Ndejembi; Katibu Mkuu Ndunguru; na timu nzima ya Ofisi ya Rais TAMISEMI; ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Mawaziri wote, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nawashukuru sana, sana kwa upendo wenu na Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa maombi yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi wa Jimbo langu la Wanging'ombe, Baraza la Madiwani, viongozi wa Serikali, wananchi wenzangu wa Jimbo la Wanging'ombe kwa maombi yao siku zote. Niwahakikishie kwamba nitaendelea kuchapa kazi kuijenga Wanging'ombe na pia kujenga Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru sana mke wangu mpenzi, Alafisa Moses Dugange kwa namna alivyokuwa karibu nami katika kipindi chote cha

matibabu. Ninawashukuru sana, sana na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nianze kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Kizazi Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo. Bajeti hiyo itatekeleza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la maabara, jengo la wazazi, jengo la upasuaji na jengo la kufulia, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Kwa kuwa kituo hicho cha Kizazi kilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi tangu 2019, mpaka sasa ni miaka mitano; na ninaishukuru Serikali kwa kutenga fedha hizo, lakini mpaka sasa hazijaanza kwenda; nataka Serikali inihakikishie: Je, ni lini kituo hicho kitakamilika ili wananchi waanze kupata huduma katika kituo hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Katika Halmashauri ya Kasulu *DC,* ipo zahanati katika Kata ya Kagerankanda, zahanati ya Uvinza ina watumishi wawili tu, tena wanaume: Je, ni lini Serikali itamwagiza Mganga Mkuu pamoja na Mkurugenzi kupeleka watumishi wa kile katika zahanati hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wa Kibondo kwa kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa kituo cha afya na ndiyo maana Serikali imetambua nguvu zao na kuweza kutenga shilingi milioni 500 ambayo itapelekwa ndani ya mwaka huu wa fedha; na mara baada ya fedha hizo kupelekwa, tunawapa maelekezo ya ndani ya miezi sita kituo cha afya kiwe kimekamilika, wananchi waanze kupata huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu Zahanati ya Uvinza katika Halmashauri ya *Kasulu DC* ambayo ina watumishi wawili wa kiume, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelichukua hilo, tutalifanyia kazi, lakini Serikali imeendelea kuajiri watumishi. Niseme, katika kipindi cha miaka miwili cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan watumishi wa afya 17,000 wameajiriwa na kupelekwa kwenye vituo vyetu na zoezi hilo litaendelea kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi na moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kujenga vituo vingi vya afya katika mkoa wangu wa Arusha na vyenye ubora wa hali ya juu, lakini changamoto kubwa ni vifaa tiba ikiwemo na kichomeataka hali inayopelekea akina mama wengi kukosa huduma ya kujifungua: Nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, napokea pongezi hizi za kazi nzuri ya Serikali. Nimhakikishie kwamba fedha za ununuzi wa vifaa tiba zimeendelea kutolewa na vifaa tiba vimesambazwa kwenye vituo, na pia mwaka huu wa fedha fedha zimetengwa kwa ajili ya vifaa tiba. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba zahanati hii itapewa kipaumbele pamoja na ujenzi wa *incinerator*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kituo cha Afya cha Makorongo kimeanza kutumika, lakini baadhi ya majengo hayajakamilika. Mfano, jengo la maabara. Nini kauli ya Serikali ya kukamilisha ujenzi huu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kituo kile kimeanza kutoa huduma za afya lakini jengo la maabara na baadhi ya majengo hayajakamilika na ujenzi huu tunakwenda kwa awamu. Nikuhakikishie kwamba Serikali inatafuta fedha kupitia mapato ya ndani lakini pia kupitia Serikali kuu ili kukamilisha majengo haya, kituo kiweze kutoa huduma vizuri zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kituo cha Afya cha Nobola kilichopo katika Tarafa ya Negezi, kimejengwa miaka mingi miaka ya 1970 na kituo hiki kimechakaa sana: Nini mpango wa Serikali wa kukarabati kituo hiki ikiwa ni pamoja na kufanya upanuzi kwa ajili ya kituo hiki? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya vituo vyote vya afya, hospitali kongwe na kuweka mpango kazi wa ukarabati kila mwaka wa fedha. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha pia katika bajeti yetu tuna fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivi vikongwe. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaelekeza Halmashauri ya Kishapu kuleta taarifa ili timu iweze kufanya tathmini na kuona mahitaji ya ukarabati na upanuzi wa kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, Serikali iko tayari kujua sababu za kwa nini Kituo cha Afya cha Iramba Ndogo hakijakamilika ili kiweze kuchukua hatua na kunufaisha wananchi kama ilivyokusudiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kufanya tathmini na kujua sababu zilizopelekea kituo hiki cha afya kutokamilika. Pia itachukua hatua za kisheria na za kinidhamu ikithibitika kuna baadhi ya watumishi ambao hawakufuata taratibu za fedha na kusababisha kituo kutokamilika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kituo cha Afya cha Kata ya Ifumbo ni kituo cha afya cha muda mrefu na kinajengwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ya kituo hiki kiweze kukamilika na Wananchi wa Ifumbo waweze kunufaika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa ujenzi wa vituo vya afya kwa kutumia nguvu za wananchi. Niwapongeze Wananchi wa Kituo cha Afya cha Ifumbo lakini tunaendelea kusisitiza kwamba kupitia mapato ya ndani watenge ile asilimia 20, 40 na 60 kwa ajili ya kukamilisha vituo hivi. Endapo halmashauri haina uwezo huo walete andiko hilo ili Serikali iweze kuchangia fedha kwa ajili ya kukamilisha kituo hicho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Kata ya Kakola kwenye Jimbo la Tabora Mjini ina jengo la mama na mtoto kwenye zahanati yao. Serikali ina mpango gani wa kumalizia boma hili ili kunusuru afya ya mama na mtoto katika Manispaa ya Tabora? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kutenga fedha kwa ajili ya kukamilsha boma hili ambalo Mheshimiwa

Mbunge amekuwa mara kwa mara analifuatilia. Fedha inayohitajika ni kidogo iko ndani ya uwezo wa halmashauri na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutafuatilia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Wananchi wa Vijiji wa Mganzi, Chagana, Nguvumoja, Ilogelo na Mwagala, Jimbo la Igunga wamekamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati; je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi kuunga nguvu za wananchi mkono? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Mbunge wa Jimbo la Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi lakini ukamilishaji unaenda kwa awamu. Tumeshafanya katika miaka miwili, mitatu yote ya fedha na tutaendelea kufanya hivyo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani lakini pia kutumia fedha za Serikali Kuu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 03

**Hitaji la Soko la Stendi – Halmashauri ya Wilaya ya Singida**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga soko na stendi ya kisasa eneo la Njiapanda Merya Halmashauri ya Wilaya ya Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida imeanza utekelezaji wa hatua za awali za ujenzi wa Stendi ya Njiapanda ya Merya. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 halmashauri ilitenga kiasi cha shilingi milioni 10 na kufanya upimaji wa eneo la stendi, kufanya usafi na kusawazisha eneo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inakamilisha tathmini ya gharama za ujenzi wa stendi hiyo na kuanza kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Halmashauri inaendelea na maandalizi ya andiko la mradi wa soko na litakapokamilika litawasilishwa Serikalini kwa ajili ya uchambuzi na endapo litakidhi vigezo litatengewa bajeti na kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu haya ya Serikali. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa soko hili pamoja na stendi ni hitaji kubwa la Wananchi wa Singida Kaskazini. Je, ni lini hasa Serikali itakamilisha hiyo tathmini ili kuweza sasa kutoa nafasi kwa miradi hii kuanza kutekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa halmashauri imeanza kutenga fedha kidogo kidogo lakini hazitoshi. Je, Serikali sasa ina mkakati gani mahsusi ya kuhakikisha inatumia vyanzo vingine vya fedha kuhakikisha ina *supplement* ili kukamilisha miradi hii kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba soko na stendi hii ni hitaji kubwa la wananchi na Serikali inatambua hili na ndio maana imeelekeza ifanyike tathmini. Tumewaalekeza Halmashauri hii ya Singida ihakikishe inakamilisha tathmini ndani ya miezi mitatu na kuleta maandiko hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili yaweze kupitiwa na kufanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali itatenga fedha baada ya kufanya tathmini, itatenga fedha kwa ajili ya kuongeza nguvu za kukamilisha ujenzi wa stendi lakini pia soko ambalo linahitajika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kufahamu ni lini Serikali itatujengea soko pamoja na Stendi ya Mkoa wa Songwe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Mkoa wa Songwe ni miongoni mwa mikoa mipya, hauna stendi lakini na soko na suala hili limekuwa likiulizwa mara kwa mara na Serikali imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi na soko katika Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo kazini na itatekeleza suala hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga Soko la Haydom na stendi yake na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulielekeza Halmashauri ya Mbulu Vijijini kufanya tathmini na kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Haydom. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kusisitiza maelekezo hayo yafanyiwe kazi na pale itakapohitajika nguvu ya Serikali Kuu basi tutakwenda kuunga mkono juhudi za ujenzi wa soko hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, je, ni lini Mradi wa *TACTIC* utaanza ili soko na stendi vijengwe Bukoba Mjini? Hili swali nimeshaliuliza zaidi ya mara tatu ndani ya Bunge hili, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeanza utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* kwa awamu ya kwanza lakini awamu ya pili pia

tathmini zinaendelea na awamu ya tatu itakwenda kutekelezwa. Kwa hiyo, Halmashauri ya Bukoba pia ipo katika moja ya awamu hizi na mradi huu utatekelezwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Kudhibiti maji yanayotuama wakati wa mvua Dar es Salaam**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu kadhia ya maji yanayotuama maeneo mengi wakati wa mvua katika Jiji la Dar es Salaam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti athari zinazotokana na mvua katika Jiji la Dar es Salaam; ikiwemo kujenga kingo za mito na mifereji mikubwa yenye urefu wa kilomita 30.7 kwa thamani ya shilingi bilioni 60 kupitia Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam *(DMDP)*.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *DMDP* awamu ya pili, Serikali inafanya usanifu na utambuzi wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa mifereji na mito yenye urefu wa kilomita 101.15, inayokadiriwa kutumia shilingi bilioni 200 katika wilaya zote za Mkoa wa Dar es Saalaam.

Mheshimiwa Spika, vilevile, *TARURA* kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* wanaendelea na

ukamilishaji wa kazi ya ununuzi kwa ajili ya uboreshaji wa Mto Msimbazi, ikiwa ni jitihada za Serikali kuendelea kukabiliana na mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme sijaridhika na jibu la Serikali.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; hivi Serikali ina mkakati gani haswa wa kuwatumia ma-*engineer* waliobobea, ma-*engineer* wa *TANROADS*, ma-*engineer* wa *TARURA* kufanya kazi ya kutatua hili tatizo ambalo ni kubwa sana kwa nchi?

Mheshimiwa Spika, pili; pesa zilizotumika ni nyingi mno kujenga barabara Mkoa wa Dar es Salaam, kujenga barabara kutoka *airport* kuja Dar es Salaam lakini maji yanayotuama yanaharibu kabisa sura ya Dar es Salaam. Serikali mnatuambia nini leo kitu cha uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa Mheshimiwa Anne Kilango, nieleze kidogo hiyo sehemu ya kwanza umesema hujaridhika na majibu na Kanuni zetu zinataka majibu yajibiwe kwa ukamilifu. Ukisema haujaridhika na jibu maana yake Serikali ije ijibu upya. Sasa nielezee hujaridhika kwa namna gani? Kwamba kuilichojibiwa hapa sicho ama hujaridhika yaani wewe unavyoona Serikali ifanye kazi. Ili nijue maswali yako ya nyongeza yajibiwe au yasubiri jibu likaloletwa sasa na Serikali.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, yajibiwe maswali yangu ya nyongeza labda nitaridhika zaidi.

**SPIKA:** Sawa. Nataka kuweka kumbukumbu vizuri za Bunge kwa sababu kazi yangu ni kusimamia Kanuni, kanuni zinataka Mbunge ukiuliza swali lako, lijibiwe kikamilifu. Sasa ukisema hujaridhika ndio nataka kujiridhisha yaani hujaridhika kwamba hii itachukua muda mrefu ili niwe nimeelewa kumbukumbu zetu zikae vizuri ama jibu lililotolewa si la kwa kweli.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, jibu lililotolewa halijanifanya niridhike. Nikipata majibu ya nyongeza ya maswali yangu, huenda nikaridhika.

**SPIKA:** Sawa. Kwa hiyo, nimekuelewa kwamba jibu iliyotoa Serikali ni jibu sahihi ila wewe ndio hujarudhika?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ni mimi ndio sijaridhika, ni sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mama yangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba Serikali kwa kiasi kikubwa ukiangalia kasi ya mafuriko ya barabarani; kwa mfano nenda Tandale, nenda Sinza, nenda maeneo mengi ya Kigogo, Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam ni mashahidi, siku za nyuma kulikuwa na mafuriko mengi sana kulikuwa hakukaliki lakini kwa sasa kuna *improvement* kubwa sana baada ya Mradi wa *DMDP* na kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusiana na mkakati wa kuwatumia ma-*engineer* wabobevu wa *TANROADS* na *TARURA* hicho ndicho ambacho Serikali inafanya. Kabla ya ujezi wa mifereji na kingo za mito, *engineer* hawa wabobevu wanafanya tathmini na kutengeneza ramani na michoro na kazi hizi zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, pia, ni kweli bado kuna changamoto kwenye barabara zetu za Jiji la Dar es Salaam kujaa maji mvua zikinyesha na ni suala endelevu ambalo inatakiwa Serikali iendelee kutenga fedha na kuendelea kwa hatua ya kujenga. Nimuhakikishie Mheshimiwa Kilango Malecela kwamba Serikali itaendelea kufanya kazi hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa mujibu wa swali hili ni kwamba maji pia hutuama katika barabara za lami ambazo nyingi zinakuwa na mashimo na hata zikitengenezwa mashimo yanajirudia pale pale.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muhimu kuwa na kitengo katika moja ya halmashauri za Jiji za Dar es Salaam kusimamia utengenezaji wa mashimo yale badala ya kutegemea kandarasi ambazo zikifanya kazi bado mashimo yanatokea tena? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina kitengo tayari cha usimamizi wa matengenezo ya mara kwa mara ya barabara zetu, yakiwemo haya mashimo ambayo yanasababisha maji kutuama. Vitengo hivyo ni Idara za Wakuu wa Idara, kwanza tuna *TARURA* kila halmashauri ya wilaya, pia tuna ngazi ya mkoa lakini pia kwenye halmashauri kuna ma-*engineer*. Kwa hiyo, wale ndio wataalamu na vitengo vile ni sahihi kusimamia.

Mheshimiwa Spika, kinachokosekana mara nyingine ni uthabiti na umakini wa usimamizi kwa vile vitengo ambavyo vina ma-*engineer* tayari. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutaendelea kusimamia kwa karibu na kuchukua hatua kwa wale ma-*engineer* ambao hawatimizi majukumu yao ipasavyo, ahsante,

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Fursa za uwekezaji**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, ni fursa gani za uwekezaji zinapatikana Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji, majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba uniruhusu nitumie dakika moja tu kutoa shukurani. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyonipa kumsaidia katika ofisi yake katika eneo la mipango na uwekezaji. Nimuahidi kwamba nitafanya kazi hii kwa bidii na utii wa hali ya juu kwake, kwa Serikali yake, kwa nchi yetu na kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa ushirikiano ambao ulinipa nikiwa Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati yako, nakushukuru sana lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano na niwaombe wanipe ushirikiano katika hatua hii ambayo ninayo kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa nijibu swali namba tano la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imejaliwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji kwenye sekta mbalimbali. Naomba nitaje sekta tano tu kwanza, katika sekta ya kilimo tunazo fursa za uwekezaji katika kuongeza thamani ya mazao. Tunayo pia fursa ya kilimo katika mazao ya kipaumbele kama vile mafuta ya kula, sukari na ngano. Tunazo pia fursa katika eneo la utalii hasa katika ujenzi wa hoteli na makazi, tunazo fursa katika eneo la viwanda hasa katika

viwanda vinavyolenga uzalishaji wa mbolea, dawa za mifugo na binadamu, nguo na mavazi na bidhaa za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la nishati na gesi tunazo fursa za uwekezaji katika kuzalishaji nishati, katika uvunaji wa gesi na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi. Tunazo pia fursa katika eneo la madini hasa katika maeneo ya utafiti, uchimbaji na uongezaji thamani ya madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni bahati kubwa kuuliza swali la kwanza kabisa kwenye Wizara mpya ya Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Serikali imefanya utafiti gani mpya na upembuzi wa kina kufahamu fursa mpya za uwekezaji zinazoendana na sayansi na teknolojia? Kama imefanya hivyo, je ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuweka taarifa hizi zinazoendana na wakati kwenye tovuti za wizara zinazotangaza masuala ya uwekezaji? Kwa sababu hata hao wawekezaji wanaangalia kwenye tovuti hizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji kila mwezi inatoa taarifa mpya ambayo inaonyesha fursa ambazo zimejitokeza. Pia inatoa taarifa kuhusu aina ya uwekezaji ambao umefanyika katika mwezi huo lakini tupokee ushauri wake kuhusu kuweka kwenye *website* ya Wizara. Nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ndio kwanza ofisi hii imeanzishwa na tupo katika mchakato wa kuanzisha taasisi mbalimbali ikiwemo suala la *website*, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kulingana na fursa mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri ameziainisha hapa zimepelekea kuwepo kwa wimbi kubwa la wawekezaji kutaka kuja kuwekeza nchini. Sasa nilitaka kujua, je, Serikali inatumia vigezo vipi kuweza kuwatambua wawekezaji wenye tija kwa Taifa hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, …

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unasubiri uitwe kwanza.

Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Nchi yetu kwa sasa inapokea idadi kubwa ya wawekezaji na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mazingira mazuri ambayo anayaweka katika kuvutia wawekezaji. Lakini tunavyo vigezo maalum vingi vya kuweza kutambua ni mwekezaji gani tumpokee na tumpeleke wapi. Naomba nitaje vitano tu;

(i) Tunahakikisha kwamba tunapokea uwekezaji ambao hatimaye utasababisha kukidhi mahitaji ya bidhaa za ndani;

(ii) Tunapendelea sana uwekezaji ambao hatimaye utaongeza thamani ili kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani ya vitu vyetu ikiwepo kwenye thamani ya mazao;

(iii) Tunaangalia uwekezaji ambao hatimaye utazalisha ajira kwa watu wetu. *(Makofi)*

(iv) Tunazingatia sana uwekezaji ambao utatusaidia kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni na;

(v) Tunazingatia sana uwekezaji ambao utadhalisha utajiri kwa watu wetu kwa hivyo kuchochea uwekezaji ndani.

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi ya vigezo ambavyo tunazingatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Katika maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ametoa, kuhusiana na maeneo ya uwekezaji ninakusudia kuzungumzia eneo la uwekezaji wa viwanda. Serikali iliwahi kutoa maelezo hapa Bungeni kwamba kumekuwa na mazungumzo kati ya muwekezaji na Serikali juu ya kujenga kiwanda cha mbolea pale Kilwa Masoko;

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatilia mazungumzo haya ili kujua yamefikia hatua gani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hebu ngoja, kabla sijamwita Waziri; umesema iko viwanda na?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliwahi kutoa maelezo hapa Bungeni kwamba pale Kilwa Masoko kuna kusudiwa kujengwa kiwanda cha mbolea itokanayo na gesi asilia ya Songosongo.

**SPIKA:** Sawa, kwa hiyo ni kiwanda kinajengwa?

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hili siyo la kwako, ni la viwanda, kwa hiyo uwekezaji huwezi kuanza kufikiri kana kwamba sekta nyingine sasa hazipo, kwa sababu la sivyo ataulizwa hadi maswali ya nishati maana nako kuna wawekezaji, ataulizwa maswali ya kila namna kwa sababu kila mahali pana wawekezaji. Lazima

aulizwe yale ambayo yanahusu mipango na uwekezaji, yale ya kisekta yanaelekea bado kwenye sekta zao.

Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dennis Londo. *(Makofi)*

Na. 6

**Ujenzi wa barabara ya Gairo – Nongwe**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Gairo hadi Nongwe itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Gairo – Labeho hadi Nongwe yenye urefu wa kilomita 54.06 kwa kiwango cha lami baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Tayari maandalizi ya nyaraka za zabuni yamekamilika na zabuni kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya usanifu zitatangazwa mwezi Septemba, mwaka huu 2023 na zitafunguliwa mwezi Oktoba, 2023. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. lakini barabara inayofanana na Gairo kwenda Nongwe ni barabara ambayo inaanzia Ruaha Mbuyuni – Malolo – Mlunga – Reli Ng'ombe mpaka Kibakwe – Mpwapwa. Barabara hii imeshapitishwa na *RCC* kwa miaka miwili sasa; Je, nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, kutokupitisha barabara hii kwa kadiri ya maombi ya *RCC* mkoa wa Morogoro; Je, Serikali haioni kwamba inawapotezea haki wananchi hawa ambao wanasafiri mwendo zaidi ya kilomita 400 kufika Mpwapwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Londo Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii inaunganisha mikoa ya Morogoro, Iringa na Dodoma na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba kwa sasa barabara hii inahudumiwa na wenzetu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini, na atakuwa pia anaelewa kwamba baada ya kupokea maombi kuipandisha barabara hii ili ihudumiwe na *TANROADS,* wataalamu wameshaitembelea ili kufanyia tathmini na kuona kama inakidhi vigezo vya kuhamishiwa *TANROADS.* Kwa hiyo tayari maombi yameshafika Wizarani kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na maamuzi, na baada ya hapo tutawajulisha kama imekidhi vigezo ili iweze kupanda hadhi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, sasa Waheshimiwa Wabunge ili tukomboe wakati Mheshimiwa Waziri unapowajibu Wabunge huna haja ya kuwataja ninakuwa nimeshawataja tayari majina yao na majimbo yao. Maswali mafupi moja kwa moja bila historia. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya kwenda Ruaha

kutoka Iringa Mjini iliahidiwa kwamba tutatangaza mwezi wa sita, mpaka sasa haijatangazwa; je, tutatangaza lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, sijamsikia barabara aliyoitaja.

**SPIKA:** Haya, kabla sijamrejeshea ili ataje hiyo barabara, hata mimi pongezi zenu na shukrani zenu kwa kuwapa nafasi nimeshazipokea, kwa hiyo hamna haja ya kuzisema, nenda moja kwa moja kwenye swali na Waziri aende moja kwa moja kwenye jibu ili tupunguze matumizi ya muda. Mheshimiwa Jackson Kiswaga taja barabara.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri mlitangaza kwamba Barabara ya kwenda Ruaha mtatangaza mwezi wa sita *tendor* hamjatangaza mpaka sasa, mtatangaza lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kulikuwa na taratibu zilikuwa bado hazijakamilika lakini zinakamilika, na baada ya hapo hiyo barabara itatangazwa ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, tarehe 5, mwezi wa Nane Wizara ilisaini barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mbingu na baadaye Mlimba. Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo itaanza kujengwa

mara tu tutakapokuwa tumekamilisha taratibu zote ikiwa ni pamoja na mkandarasi kuanza kufanya *mobilization,* yaani kuandaa vifaa kwa ajili ya kuanza kuijenga hiyo barabara. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma swali la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika; je, Serikali imefikia hatua gani katika maandalizi ya kuijenga Barabara ya Hydom – Mogitu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba arudie barabara alivyoitaja sijasikia kipande cha mwisho; Hydom?

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, Hydom – Mogitu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ilishafanyiwa usanifu na Serikali inatafuta fedha kuijenga hiyo Barabara ya Hydom Mogitu kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Msongola – Mbande kilometa 4.95, ujenzi wa kilometa 1.5 una suasua. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi huo pamoja na kilometa 3.45 za kumalizia kwa lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba tu nichukue nafasi hii kumuelekeza Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Dar es Salaam kumsisitiza mkandarasi kwa sababu yuko *site* ili barabara hiyo iweze kukamilika ili tuondokane na hiyo vumbi ambayo ina

kilomita kama 3.2. Hivyo tutakuwa tumeunganisha barabara yote kwa kiwango cha lami. Ni kumsisitiza tu meneja amsimamie mkandarasi kwa ukaribu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upembuzi yakinifu nimekuwa nikijibiwa kila mara kwamba utakamilika. Upembuzi huu ni kwaajili ya barabara kutoka Kahama – Nyangh'wale – Busisi. Je, ni lini upembuzi huo utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara hii ni ndefu na upembuzi unaendelea kadiri muda unavyokwenda, ni kwamba tu hatuwezi tukaruka hatua. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakamilisha upembuzi na baada ya hapo hatua zitakazofuata itakuwa ni kutafuta fedha kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Bugene, Nkwenda mpaka Isingiro inasababisha ajali kwa sababu ya vumbi kubwa; Je, ni lini ujenzi wake utaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante; labda tu cha kwanza ni kuhakikisha kwamba kama kuna vumbi ndiyo barabara zilivyo za vumbi, lakini Serikali imeendelea kutafuta fedha kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Pakiwa ni barabara ya vumbi haiepukiki, lakini Serikali inaendelea kutafuta fedha kuzijenga hizo barabara kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na kupunguza ajali kwenye maeneo husika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tukuyu Mjini kuna barabara ya lami inayojengwa kule njia ya kwenda Masoko, tunashukuru. Barabara ile mkandarasi ameweka kifusi kikubwa maeneo ya Ranbos kuelekea Mpindo; sasa, je, ni lini mkandarasi yule atasawazisha kifusi hicho ili wananchi wa Mpindo wapite vizuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, haya ni maelekezo tu kumuelekeza; namuelekeza Meneja wa Mkoa wa Mbeya wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba anamsimamia mkandarasi huyo kuondoa kifusi na kukisawazisha haraka inavyowezekana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Tabasam swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Kamanga – Sengerema imetangazwa kwa ajili ya ujenzi wa lami;

Je, ni lini mkandarasi atakuwa *site* kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa Barabara ya Kamanga – Sengerema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa barabara hiyo ni kwa mwaka huu kwa hiyo taratibu zinaendelea, zikishakamilika barabara hiyo itatangazwa kuanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni miezi mitatu sasa Barabara ya Masasi – Nachingwea mkataba ulisainiwa;

Je, ni lini ujenzi wake utaanza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara kama nimemsikia Masasi – Nachingwea – Liwale ni barabara ambazo ziko kwenye *EPC+F* na taratibu za kuzijenga hizi barabara zote zinaendelea, ikiwa ni pamoja na kuangalia maeneo ya kujenga makambi, kuvigawa vipande ambavyo vitatumika kujenga hizo barabara lakini pia mkandarasi kupitia upya usanifu na kuangalia fidia ambazo zitalipwa kwa wananchi ambao wataathirika na ujenzi. Kwa hiyo taratibu zimeshaanza na zinaendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante; Barabara ya Mugakorongo – Kigalama mpaka Mrongo mkandarasi alishapatikana; ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara ambazo zilitangazwa kwamba zitakuwa zimesainiwa, barabara anayoisema tayari mkandarasi alishapatikana na taratibu zinafanyika kwa ajili ya barabara hiyo, kuanzia upande wa Mrongo. Tunachosubiri sasa hivi ni kufanya *signing* na kumkabidhi mkandarasi *site* ili aanze kijenga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; Barabara ya kutoka Namtumbo – Mtonya – Mgombasi kuna daraja linalohatarisha usalama wa watu na mali zao;

Je, ni lini daraja hilo sasa litakarabatiwa katika Mto Luwegu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimuagize Meneja wa Mkoa wa Ruvuma kwenda kulitembelea hilo daraja; na kama daraja hilo halijatengewa fedha za matengenezo aweze kuleta tathmini ili tuondokane ama tusije tukapata ajali. Atuletee Wizarani gharama na tuweze kulikarabati daraja hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda sasa aulize swali lake.

Na. 7

***TANROADS* Mara kuondoa vigingi maeneo ya wananchi**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, lini *TANROADS* Mkoa wa Mara wataondoa vigingi katika maeneo ya Wananchi baada ya kushindwa kulipa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi wa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upana wa eneo la hifadhi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala ya Barabara Tanzania upo kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 1932 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1962 na baadaye mwaka 1967 ambapo lilikuwa ni mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande. Aidha, Sheria mpya ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009, ziliongeza upana wa eneo la hifadhi ya barabara kutoka mita 22.5 hadi mita 30 kila upande kutoka katikati ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wananchi ambao wamo ndani ya nyongeza ya mita 7.5 kwa nchi nzima Serikali

inaangalia upya nyongeza hii na itaandaa mapendekezo ya maeneo gani yabakie na nyongeza hii ya mita 7.5 ili fidia ilipwe na maeneo gani wananchi waruhusiwe kuendelea na shughuli zao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, katika maswali ya kuangalia sana ni hili swali. Tumeona Serikali ikiwa ikivamia wananchi kwenye maeneo yaliyovamiwa na Serikali wanabomolewa nyumba zao. Miaka 14 sasa wananchi takriban nchi nzima maeneo yale ambayo ni maeneo nyeti ya barabarani yamekaliwa na Serikali bila fidia, bila kwenda kuyapima. Sasa swali langu lilikuwa linahusu;

Je, ni lini Serikali itatoa tamko la wananchi kung'oa vila vigingi na kuingia kufanya maeneo hayo kwa shughuli za maendeleo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali imesema kwamba maeneo ambayo yamechukuliwa toka 2009 mpaka leo, kuna mengine yatafidiwa kuna mengine kuna hayatafidiwa;

Je, wale ambao hawatafidiwa wako tayari kupewa hela ya usumbufu, kwa maana ya fidia ya usumbufu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baada ya kuliona hili tatizo katika bajeti ambayo tumepitishiwa ya mwaka huu wa 2023/2024 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini, na hili linapatikana kwenye ukurasa wa 194 wa kitabu chetu. Tumeeleza hili suala na changamoto yake ambayo ipo. Na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba wale ambao wako ndani ya mita 7.5 nyumba zao hazijabomolewa; ila ziliwekwa alama ya X ya kijani ikionyesha

kwamba barabara imewafuata na wanastahili fidia. Kwa hiyo kwa sababu ya nchi nzima ndiyo maana Serikali imekuja kufanya tathmini ione ni maeneo yapi ambayo kweli sasa tutayahitaji na yatafidiwa, na yale ambayo hatutahitaji kwa sasa wananchi wataruhusiwa waendelee kuyatumia baada ya kufanya hiyo tathmini.

Mheshimiwa Spika, hao wa usumbufu nadhani sheria zetu na kanuni zetu za namna ya fidia inavyofanyika zitatumika ili kuona namna ya kuwafidia wale ambao watakuwa wamepata huo usumbufu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Mkoa wetu wa Lindi barabara zetu kuu na barabara za mikoa zina changamoto hii kubwa ya kuwepo kwa vigingi katikati ya makazi ya wananchi;

Je, ni lini Serikali italipa fidia ili wananchi waendelee na shughuli zao kama kawaida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, suala hili linafanana sana na suala la msingi na jibu langu litaendelea kubaki kwamba; ndiyo maana katika bajeti hii tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini, na kama ni maeneo ambayo tunayahitaji kwa sasa tutakuja tuwafidie halafu tuweze kujenga hizo barabara ama kuacha hiyo *corridor* ikiwa wazi baada ya kuwaondoa wananchi kwa kuwafidia likiwa ni pamoja na hilo la eneo la Mheshimiwa Mbunge ambalo amelisema. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu lilikuwa ni swali la namba sita sasa sijui kama utaniruhusu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita ujumbe ninao hapa mbele unasema, sita au saba. Maana yake umenipa mimi uchaguzi; kama unauliza hapa ni fidia, kama halihusu fidia swali namba sita limeshapita.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna baadhi ya maeneo unakuta kwamba jiwe la *TANROADS* limewekwa zaidi ya mita 30 kama ambavyo umetuhabarisha hapo;

Je, katika mazingira hayo *TANROADS* watakuwa tayari kuondoa mawe hayo kwa gharama zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kama ni barabara ambayo imesanifiwa maana yake ni kwamba pale ilipo ndipo zinapoishia mita 30, na maana yake ni kwamba pale ilipo barabara ambayo ipo itasogea upande huo ili kufikisha mita 30. Hao watakuwa watafidiwa pia kwa sababu barabara itakuwa imehama kutoka ilipokuwa na kusogea upande huo wa kwenye kigingi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage. *(Makofi)*

Na. 8

**Ujenzi wa Ofisi ya Wilaya ya *TANESCO* Kibiti**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Ofisi ya Wilaya ya *TANESCO* – Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu: -

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa umahususi na umuhimu wa Wilaya ya *TANESCO* Kibiti, *TANESCO* inafanya tathmini ya gharama kuangalia namna ya kujenga jengo lake la ofisi ili kuepuka kuendelea na ofisi iliyopo sasa ambayo ni ya kupanga.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na maendeleo makubwa ya teknolojia, kwa sasa huduma nyingi zinatolewa kwa njia ya mtandao. Aidha, programu kama vile NIKONEKT, NIHUDUMIE, kununua umeme (LUKU) na nyinginezo zimeanzishwa ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wateja bila kulazimika kwenda ofisi za *TANESCO*. Aidha, pamoja na faida nyingine programu hizi zimesaidia kuondoa vishoka waliokuwa wanawalaghai wateja katika ofisi za *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, shirika limeelekeza fedha nyingi katika kuanzisha na kuboresha huduma zinazotolewa kwa njia ya mtandao. Sambamba na hili, shirika linaendelea kuanzisha viunga/ofisi ndogo zitakazokuwa karibu zaidi na wananchi ili kuwahudumia kwa haraka kwa huduma chache ambazo hazipatikani kwa mtandao kwa sasa. Katika Wilaya ya Kibiti, *TANESCO* imeanzisha viunga viwili katika maeneo ya Hanga na Bungu ili kusogeza huduma kwa wateja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage Swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na maelezo mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kweli anasema kuna mitandao ambayo inatumika kuhudumiwa na *TANESCO* lakini Kibiti ni moja ya mkoa ambao uko Kusini mwa Mkoa wa Pwani ambapo kuna mikoa minne; Mkuranga, Mafia pamoja na Rufiji. Sasa hatuoni umuhimu wa kujenga kituo kikubwa sana kwa sababu hapo ni *centre* ya mikoa ya Kusini ya Mkoa wa Pwani, kituo kikubwa ambacho wananchi wataweza kufika sababu sio vijiji vyote ambavyo wanaweza kufikiwa na mambo ya mtandao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, tunaendelea kufanya tathmini kwenye *paragraph* ya kwanza. Nimesema kwa umahususi wa Kibiti kwa ajili ya kuona namna ambavyo tutafanya ili kujenga ofisi hii ili iweze kuhudumia maeneo ya Kibiti lakini na maeneo mengine ya Jirani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Miji wa Iringa ni kivutio cha utalii Kusini na katikati ya mji tumeboresha sana majengo yetu. Kuna jengo la *TANESCO* la Ofisi ya Mkoa ambalo limetelekezwa muda mrefu, ni lini mtalimalizia ili liendelee nalo kuchangia uvutiaji wa Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika maeneo yote ambayo majengo hayajakamilika ni swala la kibajeti na tunaendelea kujikusanya kwenye fedha na kutanguliza vipaumbele lakini nimhakikishie Mheshimiwa Jesca kwamba jengo

hilo pia litakamilishwa ili liweze kuwahudumia wananchi lakini kama ulivyosema liwe kivutio cha utalii Iringa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu na hivyo kusababisha changamoto ya kupata huduma kwa wakati. Lini sasa Serikali inampango wa kuanzisha Mkoa wa ki-*TANESCO* katika wilaya ya Kahama ili isaidie kutoa huduma kwenye maeneo yale? Ahsante.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kassim Iddi swali linahusu jengo, unataka lianzishwe jengo na wakati huo huo Mkoa?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa namaanisha ianzishwe Ofisi ya Kimkoa wa Ki-*TANESCO* Kahama, sio jengo.

**SPIKA:** Haya, swali la msingi linahusu Jengo la Ofisi ya *TANESCO*. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu: -

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kweli Wilaya ya Kahama inazo Halmashauri tatu na sisi tunayo Ofisi ya Kiwilaya ya *TANESCO* kama zilivyokuwa ofisi nyingine za Serikali na tunachokifanya ni kuendelea kupeleka huduma kwa wananchi kwa kufungua ofisi ndogo au viunga kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kufungua Ofisi ya Kimkoa ya Ki-*TANESCO* tunaendelea kulitizama kwa sababu zinazo viwango na *grade* mbalimbali na zitakapokuwa zimekamilika tutakamilisha jambo hilo kwa ajili ya huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Makete sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Kuitangaza Hifadhi ya Taifa Kitulo**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Kitulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuitangaza hifadhi ya Taifa Kitulo Kitaifa na Kimataifa kwenye maonyesho na matamasha mbalimbali kama vile Karibu Kusini, Kili-*fair*, Sabasaba, na Nanenane. Pia, tumeanza kuitangaza kwa njia ya kidigitali, mitandao ya kijamii, majarida na *Safari Channel.* Lengo ni kuvutia watalii na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeanza kuboresha miundombinu ndani ya hifadhi ikiwemo ujenzi wa nyumba tatu na tunatarajia kujenga nyumba mbili na kambi moja ya kuweka hema katika mwaka huu wa fedha wa 2023/2024, pamoja na kukarabati miundombinu ya barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, licha ya majibu mazuri ya Serikali ya kuitangaza Hifadhi ya Kitulo lakini Serikali ina mradi wa *regrow* mradi ambao umejikita kwenye kutangaza utalii Kusini mwa Tanzania na hifadhi hii ni hifadhi ya kipekee Barani Afrika na Tanzania, kwa nini mradi *regrow* haujaenda kwenye Hifadhi ya Kitulo ili uweze kuisaidia hifadhi hii kutangazwa kwa ukubwa zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye Hifadhi ya Kitulo kumekuwa na changamoto ya kimahusiano kati ya wananchi na hifadhi kwa maana ya migogoro ya mipaka. Sasa katika jitihada za kutangaza utalii ni upi mkakati wa Serikali kutatua migogoro iliyopo kwenye vijiji vya Misiwa, Ujuni, Nkondo, Makwalanga, Lugoda na Igenge. Vijiji hivi kwa muda mrefu vimekuwa na mgogoro na hifadhi, upi mkakati wa Serikali kutatua mgogoro huu ili mahusiano yaweze kuimarika kati ya hifadhi na Wananchi wa Wilaya ya Makete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Festo Richard Sanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa miradi ya *regrow,* mradi wa *regrow phase one* ulikuwa unawezesha kufanya maboresho katika hifadhi nne ambazo ilikuwa ni Mikumi, Nyerere, Udzungwa na Ruaha, lakini Serikali inatarajia kuingia mkataba tena kwenye *REGROW Phase Two* ambayo Hifadhi ya Kitulo pia itaingizwa katika mradi huo. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Kitulo itaingizwa kwenye *phase two* na maboresho yatafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa migogoro tulishapeleka tathmini tayari ilishafanyika na sasa hivi ni utekelezaji tu wakuainisha mipaka mipya. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa naomba nielekeze tu *TANAPA* waende kuweka vigingi katika maeneo ambayo yameainishwa baada ya tathmini kuwa imefanyika lakini na sisi pia tutaenda kujihakikishia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda Mbunge wa viti maalum sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Ugumu wa kupata mikopo wanafunzi waliosoma shule binafsi**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Aliuliza: -

Je, kwa nini kumekuwa na ugumu wa upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi waliosoma shule binafsi wanapojiunga na elimu ya juu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga majibu: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda kama ifuatavyo: -

Mheshimwa Spika, mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inawalenga vijana wenye sifa za kitaaluma za kujiunga na taasisi za elimu ya juu lakini hawana uwezo wa kumudu gharama za elimu.

Mheshimwa Spika, aidha, upangaji na utoaji mikopo unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo Sura 178 kwa kuzingatia sifa za msingi ambazo ni: awe Mtanzania; awe amepata udahili wa masomo ya shahada au stashahada katika taasisi inayotambuliwa na Serikali; asiwe na vyanzo vingine vinavyogharamia masomo yake; na kwa wanaoendelea na masomo ya mwaka wa pili, watatu na kuendelea, wawe wamefaulu kuendelea na masomo yao katika mwaka unaofuata.

Mheshimwa Spika, Kila mwaka bodi huandaa mwongozo unaopaswa kuzingatiwa na waombaji na kuweka masharti ya utoaji mikopo kwa mwaka husika. Pamoja na vigezo vilivyotajwa, mwongozo hueleza taratibu za kufuata wakati wa kuomba mkopo pasipo kuangalia mwanafunzi kasoma shule ya binafsi au ya umma.

Mheshimiwa Spika, iwapo muomboji atafuata maelezo yote kama yalivyo katika mwongozo wa mwaka husika na akawa ana vigezo vyote, hatutegemei pawepo na ugumu wowote katika kupata mkopo hata kama alisoma shule binafsi. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Shule binafsi ni wadau wakubwa sana wa elimu katika Taifa hili la Tanzania lakini imekuwa mara nyingi vijana hawa wakifika elimu ya juu wanakosa mikopo au kupata chini ya 40% hatuoni kwamba tunawaonea, watoto wengine wamesomeshwa kwa msaada wakiwemo yatima, kuwazuia kuendelea na elimu ya juu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali haioni sasa kuna umuhimu watoto wa nchi hii wote wapate mikopo *flatrate* yani mikopo ya aina moja bila kugawa kwa asilimia ili watoto wote wapate usawa katika Taifa hili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Mwakagenda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba utoaji wa mikopo yetu hauzingatii mwanafunzi amesoma katika shule gani, iwe shule ya umma au shule ya Serikali ilimradi wamekidhi vile vigezo wanafunzi hao wanawajibika kupata hiyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na changamoto wakati mwingine wakupata asilimia chache sana ya mikopo hii. Tunafahamu kuwa juhudi za Serikali zakuongeza wigo wa kupata mikopo hii kwa kuzingatia bajeti yetu ya Serika bado zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu Serikali imeendelea kuongeza fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 464 mwaka 2021/2022 mpaka shilingi bilioni 738 mwaka 2023/2024. Ni matumaini yetu kuwa ongezeko hili la bajeti litahakikisha kwamba wanafunzi wengi wanapata mikopo na kwa kiasi kikubwa cha mikopo.

Mheshimiwa Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, vilevile Serikali imeendelea kufanya juhudi ya kutafuta wadau mbalimbali wa kuweza kuongeza nguvu. Mpaka sasa tunavyozungumza taasisi yetu ya Benki ya NMB katika mwaka wa fedha uliopita iliweza kutenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya mikopo hii. Na katika mwaka huu vilevile itatenga fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ikiwa ni kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi wa elimu ya juu anapata mkopo na anapata mkopo katika kile kiasi ambacho kinahitajika. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati ambao wanapata *diploma* na vyeti hapa nchini kwetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Saputu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ya 2023/2024 jambo hili lilizungumzwa bayana katika Bajeti Kuu ya Serikali. Serikali imetenga fedha kwa ajili ya utoaji mikopo kwa vyuo hivi vya kati na *programme* hii itaanza mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri huoni umuhimu sasa wa Serikali kufanya mapitio ya sheria ya hii Bodi ya Mikopo ili kuweza kutatua changamoto nyingi ambazo watoto wa Kitanzania wanazipata kupata mikopo ya elimu ya juu? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Tweve kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mradi wetu wa *Higher Education for Economic Transformation* tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya mapitio. Tunafahamu sheria hii ya Bodi ya Mikopo imeanza toka 2004 ni miaka 19 sasa toka sheria hii ianze. Kwa hiyo, hivi sasa tunafanya mapitio ili kuangalia vigezo namna gani ya kuweza ku-*update information* zetu lakini vilevile namna ya utoaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuondoe wasi wasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu mpaka kufika mwisho wa mwaka huu wa fedha shughuli hii itakuwa imekamilika na bodi yetu sasa itakuwa na sheria pamoja na miongozo ambayo itaendana sawa na kasi ya sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato swali la nyongeza.

**MHE. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuwapatia mikopo wanafunzi wote wenye ulemavu wa aina yoyote katika vyuo vyetu vikuu kwa 100%?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Nahato kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kigezo kimoja wapo cha wanafunzi kupata mikopo ni wale wenye ulemavu naomba nimuondoe wasi wasi Mheshimiwa Mbunge watoto wetu vijana wetu wenye ulemavu wanapata mikopo kwa 100% na huo ndiyo mpango wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini sasa Serikali itaanzisha *revolving fund* ikiwa na maana kwamba zile fedha zinazokusanywa ziwekwe kwenye mfuko ambao ni fedha lindwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wambura amezungumzia swala la *revolving fund* kama nilivyoeleza kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Tweve nadhani kwamba hivi sasa tunafanya mapitio ya sheria ile. Katika mapitio yale tutakwenda kuangalia hayo mambo yote pamoja na kuangalia kama mfuko unaweza kujiendesha lakini vilevile katika kujiendesha katika taratibu za kibenki ikiwemo na hii *revolving fund*. Kwa hiyo, nimuondoe wasi wasi jambo hili linafanyiwa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, *NMB* kama mdau wa elimu ameandaa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu lakini mikopo hii itatolewa kwa wale wanafunzi ambao wazazi wao ni wafanyakazi. Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha wale wanafunzi wanaohitaji mikopo ambao wazazi wao siyo watumishi wanapata mikopo kwa asilimia zote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Migilla kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli wenzetu wa *NMB* walitenga fedha shilingi bilioni 200 katika mwaka wa fedha uliopita na mwaka huu watatenga tena kwa ajili ya kuendelea na zoezi hili. Nimuondoe wasi wasi Mheshimiwa Mbunge pamoja na kigezo kile cha mzazi awe ni mtumishi lakini vilevile tumeweka kigezo cha mzazi kuwa mkulima. Ilimradi amejiunga au yupo ndani ya chama cha ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wazazi wote ambao ni wafanyakazi lakini wazazi wote ambao ni wakulima au wale ambao wako katika vyama mbalimbali wanahusika na mikopo hii na tutakwenda kufanya *review* kwa kadiri mahitaji yatakavyohitajika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hili swala la mikopo lina changamoto hasa pale mtoto wa masikini anapokosa hata ile asilimia ndogo haipati au anapata 40% na 60 hawezi kuipata. Katika huu mchakato wenu mnaoendelea nao ambao mnatazama upya jambo hili mtazame namna wakati mnatenga zile fedha zitengwe fedha kiasi kwa ajili ya wale Watoto ambao mfumo unakuwa haujawatambua lakini kwa kweli wanashida.

Haijalishi popote aliposoma hoja ni kwamba mzazi anashida. Mwingine anaandika mzazi wangu ana kazi lakini hiyo kazi anapata mshahara wa laki moja yeye ni mfagizi. Ni mfanyakazi kweli lakini ni mfagizi ataweza kulipa ada kweli ya huyo mtoto?

Kwa hiyo, kesi kama hizi zipo nyingi wakati mnatazama huu mfumo mtazame namna ya kutenga fedha kwa ajili ya hawa watoto ambao mfumo unakuwa umeshindwa kuwatambua wanapokuja kwenu muweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 11

**Hitaji la hosteli kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu Morogoro**

**MHE. NORAH W. MZERU** sliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la uhaba wa Hosteli kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu wanaosoma katika Vyuo vya Mkoa wa Morogoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA,** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya juhudi mbalimbali katika kutatua tatizo la uhaba wa hosteli kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vikuu hapa nchini vikiwemo Vyuo vya Mkoa wa Morogoro. Kwa sasa hosteli zilizopo katika vyuo vikuu vya Mzumbe na Sokoine zina uwezo wa kulaza jumla ya wanafunzi 7571. Ikiwa Mzumbe ni wanafunzi 3742 na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ni wanafunzi 3829.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wanafunzi ambao hawapati nafasi za malazi katika hosteli za vyuo wamekuwa wakipata malazi katika hosteli zinazomilikiwa na watu binafsi katika maeneo yaliyokaribu na vyuo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ongezeko la uhitaji wa malazi kwa wanafunzi katika vyuo vikuu vya serikali vikiwemo vyuo vya Mkoa wa Morogoro, Serikali imekamilisha ujenzi wa hosteli 4 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1024 katika Chuo Kikuu cha Mzumbe na zimeanza kutumika kuanzia mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation* yaani *HEET* imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli moja yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 katika

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Kampasi ya Mazimbu Morogoro. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali itawasaidiaje wamiliki wa nyumba za kulala wenye nia ya kubadilisha matumizi na kuzifanya *hostel* hasa katika suala la tozo za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mzeru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kubadilisha matumizi ya nyumba pamoja na ardhi yapo kwa mujibu wa sheria, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu hizo wamiliki wa nyumba pamoja na ardhi wanapaswa kuzifuata, lakini kwa vile wanafanya biashara ni lazima zile taratibu zingine za tozo pamoja na kodi ya Serikali ni lazima zilipwe. Kwa hiyo, ni muhimu kwa wale wamiliki wanapobadilisha matumizi kwenda kwenye mamlaka husika kutoa taarifa ya kubadilisha zile leseni zao za biashara ili waweze kupata tozo ambayo ni sahihi. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia utaratibu wa ubia na sekta binafsi katika kujenga mabweni kwenye Vyuo na hata kwenye Sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kimei kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kimei ametoa wazo, naomba tulichukue ushauri wake tuende tukaufanyie kazi ili tuweze kuangalia ni nimna gani tunaweza tukajenga hosteli kwa njia ya *PPP*. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Kuwasaidia wanawake na vijana wachimbaji wa madini – Lulindi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawasaidia wanawake na vijana wa Kata za Mitesa na Nanjota wanaojihusisha na uchimbaji madini Lulindi?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara umebarikiwa kuwa na madini mbalimbali yakiwemo madini ya ujenzi ambayo huchimbwa zaidi na wananchi hasa wanawake na vijana. Aidha, Tume ya Madini imetoa leseni za uchimbaji madini ya ujenzi na chumvi kwa vikundi 11 vya wanawake na vijana. Vikundi hivyo ni pamoja na *Mtazamo Group, Wazawa Group, Mwambani Group, Wasikivu, Songambele Group,* Tusaidiane, *Nguvu Kazi Youth Group* katika Halmashauri ya Mji wa Masasi na Kikundi cha Kiumante kilichopo katika Manispaa ya Mtwara – Mikindani; Vikundi vya *Makonde Salt Group,* Mapinduzi na Umoja wa Vijana vilivyopo katika Halmashauri ya Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuwasaidia wanawake na vijana wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini katika Kata za Mitesa na Nanjota, tunawashauri Wanawake na Vijana wajiunge kwenye vikundi na kusajiliwa katika Halmashauri husika. Kufanya hivyo itakuwa rahisi kuwahudumia na kuwasaidia kupatiwa leseni za uchimbaji na mikopo kutoka Halmashauri husika na hata mabenki.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini tutaendelea kutoa elimu kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kujiunga katika vikundi ili kuweza kupatiwa huduma kwa ufanisi na kwa haraka zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kutokushiriki kikamilifu kwa vijana na wanawake katika shughuli hii ya madini ni mikopo kwa maana ya *capital*.

Je, Serikali haioni sababu ya kuwapa vijana mitaji ili kusudi washiriki kikamilifu katika sekta hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mchungahela mtetezi makini wa watu Jimbo la Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli changamoto kubwa ya vijana, wanawake na wachimbaji mbalimbali ni ukosefu wa mitaji. Katika kutanzua changamoto hii Wizara ya Madini kupitia Shirika lake la Taifa la Madini *(STAMICO)* wamewaweka wakfu walezi wakuu wa wachimbaji wadogo na hatua za awali za kuwasaidia zimehusisha kutoa elimu ili wafahamu namna ya kufanya uchimbaji wa tija, Sheria ya Madini, pia kuingia katika makubaliano na taasisi za kifedha hapa nchini zikiwemo Benki za NMB, CRDB na Azania ili waweze kuwakopesha wale ambao wamekidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, ili waweze kusaidiwa, wananchi wa Jimbo lake na Watanzania wote ambao wamepata hamasa ya kujihusisha na biashara ya madini ni vizuri waunde vikundi ili kuwa rahisi kuwafikia na kuwasaidia kupitia vikundi na wajiunge na Chama cha Wachimbaji wadogo wa Madini Tanzania ambao sasa hivi wapo kwenye mchakato wa kuanzisha benki yao ili waweze kupata mitaji na waweze kuchimba kwa wakati kwa tija zaidi na wa ufanisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi Mbunge wa Moshi Vijijini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 13

**Changamoto za wakulima waliowekeza kwenye *SACCOS* – Moshi Vijijini**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua changamoto za wakulima waliowekeza kwenye *SACCOS* na fedha zao kupotea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa upotevu wa fedha za wanachama wa *SACCOS* nchini unadhibitiwa ipasavyo, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika inayo mikakati mbalimbali, ikiwemo kutoa miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchi zikiwemo *SACCOS*, kuanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), ambao utasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji

katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Vyama vya Ushirika, zikiwemo *SACCOS*, kuendelea kutoa elimu ya ushirika kuhusu namna bora ya uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa wananchi wote, wakiwemo wanachama, viongozi na watendaji wa *SACCOS* kupitia njia mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili katika Jimbo la Moshi Vijijini limekuwa kubwa sana; je, Naibu Waziri upo tayari kuambatana na Profesa Ndakidemi kwenda kutatua changamoto hiyo?

Swali la pili, katika Jimbo la Hai *SACCOS* ya Kware, *SACCOS* ya Lyamungo, Masama Mula, Mudio na Lemira, wananchi walihamasishwa kujiunga na *SACCOS* hizi baadae viongozi wale walitoroka na fedha za wanachama.

Je, ni lini Serikali itakwenda katika Wilaya ya Hai kutatua changamoto hizi ikiwa ni Pamoja na kurudisha fedha za wanachama wa *SACCOS* nilizozitaja?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika Jimbo lake kuangalia changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, natumia fursa hii kumuelekeza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika kuhakikisha kwamba anatuma timu yake kwenda kufanya uchunguzi wa awali juu ya jambo hili na baadaye hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wale wote ambao wametoweka na fedha za wanachama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Kuwa na kiuatilifu kimoja kwenye zao la korosho**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, ni lini kutakuwa na kiuatilifu kimoja cha magonjwa kwenye zao la korosho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika zao la korosho kuna magonjwa makuu manne ya ubwiriunga, blaiti, chule na debeki yanayodhibitiwa kwa viuatilifu vyenye viambata amilifu tofauti.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa visumbufu vya mazao, Serikali itaendelea kuimarisha utafiti na kushauri wakulima kutumia viuatilifu vyenye tija zaidi katika kilimo. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu inaendelea kupitia upya usajili wa viuatilifu vyote ili kubaki na viuatilifu vinavyofaa sokoni kulingana na aina ya zao, eneo na magonjwa yaliyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kumekuwa na ongezeko au utitiri wa viuatilifu vita kwenye zao la korosho; je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kutoa elimu kwa wakulima wakati wa ugawaji wa viuatilifu hivi?

Swali la pili, naipongeza Serikali kwa kuanza mfumo wa usajili wa wakulima wa korosho ili kutoa pembejeo na viuatilifu kwa wakulima lakini kuna kundi kubwa la wakulima ambao mpaka sasa hawajasajiliwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya usajili kwa wakulima hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la utitiri wa viuatilifu, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi viuatilifu hivi huwa vinatokana na aina ya magonjwa vilevile wadudu waharibifu ambao wanapelekea matumizi ya viuatilifu hivyo. Jambo kubwa ni kwamba kama Serikali kupitia kituo cha utafiti cha *TARI*-Naliendele pamoja na Bodi ya Korosho tutaendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu hivi ili mwisho wa siku viweze kuleta tija na tuongeze uzalishaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu usajili wa wakulima. Zoezi la usajili wa wakulima linaendelea. Ni kweli wapo baadhi ya wakulima bado hawajasajiliwa, tunaongeza nguvu kupitia bodi kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya rasilimali watu ambao watasaidia kufanikisha zoezi la usajili huo wa wakulima ili wakulima wote waweze kusajiliwa na wapate viwatilifu kwa wakati kwa sababu hivi sasa ni takwa la lazima kwamba wakulima tuwe tumewasajili ili waweze kupata viuatilifu kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tunaongeza jitihada kubwa kuhakikisha kwamba zoezi hili linakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako. Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri kuna Mbunge kumbe amesimama, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na kusema kwamba tusitoe pongezi naomba uniruhusu

nitoe pongezi kwa Serikali kuhusiana na suala zima la zao la mbaazi. Mbaazi tulikuwa tunauza kilo mpaka shilingi 100 lakini kwenye mnada wa mwisho tumeuza shilingi 2,130. Haya ni mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Serikali, je, bei hii itakuwa ni endelevu ili kuhakikisha kwamba wakulima wanaongeza uzalishaji wa zao hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wanaendelea kunufaika na kilimo. Tutahakikisha tunaendelea kuweka miundombinu rafiki ili bei hii iendelee kumnufaisha mkulima na hasa wakulima wa mbaazi kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde sasa aulize swali lake.

Na. 15

**Uhakika wa hesabu zinazowasiliswa Serikalini**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliauliza: -

Je, hesabu zinazowasilishwa na CAG kila mwaka ni za mashaka au uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Said Issa, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hesabu zinazowasilishwa na Maafisa Masuuli kwa *CAG* kila mwaka ni za uhakika kwa kuwa zinaandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 30(2) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (*IPSAS*), miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara ya Fedha na mifumo madhubuti ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha ikijumuisha Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2019/2020 – 2021/2022), taarifa ya *CAG* imeonesha ongezeko la hati zinazoridhisha kutoka asilimia 92 mpaka 96 kwa Serikali Kuu, asilimia 70 mpaka 94 kwa Serikali za Mitaa na kupungua kutoka asilimia 97 mpaka 98 kwa Mashirika na Taasisi nyingine za Umma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, wale waliokutwa na ubadhirifu wamechukuliwa hatua gani?

Swali la pili, je, Serikali itakuwa tayari kuweka utaratibu wa kuutangazia umma wale waliochukuliwa hatua pamoja na hatua zilizochukuliwa ili kuwafanya Watanzania waweze kuiamini Taasisi hii ya *CAG*? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, tunalipokea wazo la Mheshimiwa Mbunge na hivi ndivyo ambavyo tumekuwa tukifanya kwamba wale ambao wanabainika kuwa na makosa wanachukuliwa hatua. Mpaka sasa kuna hatua mbalimbali ambazo zinaendelea baada ya taarifa ya *CAG* kukamilika. Baada ya majibu ya Serikali kutolewa yale maeneo yanayoonekana kuwa na hatia ndani yake yanakwenda kwenye uchunguzi na sasa hivi tuna majalada ambayo yako ngazi ya uchunguzi na tuna yale ambayo yalishafika ngazi za kimahakama. Pia kuna maeneo ambayo kesi

zilishahukumiwa ambazo zinahusisha upotevu ambao taarifa zake zimepatikana kupitia taarifa ya CAG.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutangaza tumepokea hilo, tutaboresha vitengo vya mawasiliano ili vianze kutoa matamko kwenye maeneo ambayo hatua zimechukuliwa pale ambapo kulikuwa na ubadhirifu umebainika kupitia taarifa ya CAG.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Kuongeza thamani ya shilingi ya Tanzania**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuza: -

Je, kuna mpango gani wa kuongeza thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na nchi jirani za Afrika Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kulinda thamani ya shilingi ya Tanzania kwa hatua zifuatazo:-

(i) Kushirikisha sekta binafsi katika kuimarisha mikakati ya kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi;

(ii) Kuhimiza wananchi kuongeza matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini ili kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni;

(iii) Kusimamia kwa karibu wazalishaji wa ndani ili kuongeza ubora katika uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa lengo la kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi;

(iv) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa kifungu 7(3) na 13(1) cha Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 2022, zinazoelekeza wafanyabiashara kuweka katika benki zilizopo nchini fedha za mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ndani ya siku 90 tangu siku ya kusafirisha bidhaa au kutoa huduma na wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka nje kufanya malipo kwa kutumia benki na taasisi nyingine za fedha zilizopo nchini;

(v) Kuongeza vyanzo vya upatikanaji wa fedha za kigeni ikiwemo ununuzi wa dhahabu;

(vi) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji kutoka nje; na

(vii) Kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha ili kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS HENRY MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, anafahamu usumbufu wanaoupata wafanyabiashara kwenye mipaka yetu, kwa maana ya mipaka ya Kenya na Rwanda, kwa vile kule kila wakati faranga inapanda bei na kushuka lakini shilingi nakumbuka mwaka 1995 enzi za Mkapa ndiyo shilingi ilipanda bei na hii ndiyo inachangia ugumu wa maisha.

Sasa kuna mkakati gani wa kuifanya shilingi yetu iwe na thamani ili wananchi waweze kupata bidhaa kwa bei nafuu kulingana na upandishaji wa thamani?

Swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mfumuko wa dola, kwa sababu kumekuwa na kupanda sana kwa dola bila

utaratibu. Leo unakuta dola inabadilishwa kwa shilingi 2,550 lakini jioni ukienda tena unakuta inabadilishwa kwa shilingi 2,800 na hii inafanya Taifa kuwa na maisha magumu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kumjibu Mheshimiwa Mbunge maswali yake mawili ya nyongeza. Moja, Serikali imejitahidi kusimamia kuhakikisha la kwanza, thamani ya shilingi haishuki; la pili, ambalo tunalifanya katika mikakati yote hii ambayo unaiona Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu aliyoielekeza ya kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji, malengo ya muda mrefu kwenye hilo ni kwenda kuimarisha, kuongeza thamani ya shilingi yetu. Tutaongeza thamani ya shilingi yetu kwa namna nyingi zikiwemo hizo mbili za kuongeza mauzo nje ili tuwe na dola nyingi. Pili, kwa kuzalisha bidhaa ambazo tunaweza tukajitegemea na tukatumia ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti mabadiliko ya haraka haraka ya bei ya dola, Mheshimiwa Mbunge, katika kipindi cha muda mfupi, tunalishughulikia jambo hili ili kuweza kukabiliana na tatizo ambalo limejitokeza la dunia nzima la upungufu wa dola, ambapo hicho ndicho kinachosababisha mahitaji ya dola yanakuwa makubwa kuliko upatikanaji wa dola na hivyo kufanya bei ya dola kuanza kubadilikabadilika.

Mheshimiwa Spika, hata sasa tuna hatua ambazo tumeendelea kuzichukua ambazo tunaamini zitaweza kusaidia dola ziwepo nyingi sokoni, na zikiwa nyingi sokoni zitasababisha tatizo la bei kubadilikabadilika kuweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, tunatoa rai kwa wadau wote wanaoshiriki katika soko la kubadilisha fedha, waendelee kushiriki kikamilifu ili kuweza kuhakikisha kuwa Dola haiadimiki sokoni na hivyo kusababisha bei kubadilikabadilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Tamina Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Ukarabati wa nyumba za askari – Kaskazini Unguja**

**MHE. TAMINA HAJI ABASS** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kukarabati nyumba za makazi ya Askari Polisi Kaskazini Unguja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tamina Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tathmini kwa ajili ya ukarabati wa nyumba zote 14 za makazi ya askari polisi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, imefanyika na kiasi cha shilingi 447,065,000 zinahitajika. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye Bajeti ya Serikali ya 2024/2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tamina Haji Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMINA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya matumaini ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile fedha hizo zitatengwa kwenye bajeti ya mwaka ujao; je, itawasaidiaje askari wanawake ambao wanaishi mbali na vituo vyao vya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imeelezwa, nyumba hizi 14 zitakapokarabatiwa, mgao wa nyumba hizo kwa Askari wetu uzingatie uwiano wa jinsia ili Askari wa kike ambao Mheshimiwa ana mashaka kwamba wanakosa nyumba za kuishi waweze kupata nyumba, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya kukubali ombi letu la wananchi wa Jimbo la Chumbuni kutupa ruhusa ya kujenga kituo chetu kikubwa cha Polisi ambacho tunaendelea nacho hivi sasa. Kama swali la msingi lilivyoulizwa kuhusu matatizo ya makazi, nasi tunatarajia kuwa na kituo kikubwa cha *Class C;* je, anatuahidi nini katika tatizo hili la makazi kwa sababu tunajenga kituo kikubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunaweka kipaumbele na kila tunapojenga kituo kikubwa cha polisi, tunazingatia pia makazi ya askari na viongozi wa Jeshi la Polisi. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Mbunge, ni kuhakikisha linapatikana eneo ili mpango wa ujenzi uende sambamba na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za vijana wetu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, sasa aulize swali lake.

Na. 18

### Mazoezi ya uokozi wa ajali majini Kivukoni – Kigamboni

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza: -

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kufanya mazoezi ya utayari katika uokozi wa ajali majini katika Kivuko cha Kivukoni – Kigamboni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina boti moja ya maokozi iliyopo katika Daraja la Mwalimu Nyerere iliyopo Ofisi ya Mkuu wa Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kigamboni ambayo hutumika kwa ajili ya maokozi ya ajali za majini katika Bahari ya Hindi na kwenye fukwe zote za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeandaa na kutekeleza mkakati wa utoaji wa elimu na mazoezi katika Wilaya ya Kigamboni kwa kushirikiana na Ofisi ya kivuko cha Magogoni – Feri, *Kigamboni Beach Management Unit (BMU)* na wavuvi kwa ajili ya utayari wa huduma ya uokoaji wakati wa ajali za majini katika Kivuko cha Kigamboni na maeneo mengine ya jiji. Mkakati huo unatekelezwa pia kwenye sehemu zote zenye bahari kuu, maziwa makuu na mito ikiwemo Mkoa wa Pwani, Mara, Kagera, Geita, Kigoma na Mwanza, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu haya ya Serikali. Katika dhana hiyo ya utayari katika masuala ya uokozi, Wilaya ya Kigamboni ina matanki makubwa ya mafuta na hatuna gari ya zimamoto wala Kituo cha Zimamoto.

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunakuwa na Kituo cha Zimamoto na gari la Zimamoto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina mpango wa kuendelea kuimarisha Jeshi letu la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vifaa na utaalam ili kutekeleza majukumu hayo. Kama mazungumzo yetu na wakopeshaji yataenda vizuri, tunaweza kupata magari zaidi ya 150 kwa ajili ya shughuli za Zimamoto na Uokozi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya Kigamboni ambayo Mheshimiwa amefanya marejeo yake na umuhimu wa uwekezaji uliopo pale hasa matenki ya mafuta, kipaumbele kitawekwa kuhakikisha kwamba kunapatikana magari ya kuzima moto na kuimarisha Ofisi ya Zimamoto upande wa Kigamboni ili kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Huduma ya M-Mama kwa wajawazito**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuhimiza mashirika mengine ya simu kujiunga na mpango wa M-Mama kwani umekuwa msaada kwa wajawazito wengi?

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa M-mama unatekelezwa na kusimamiwa na Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya

*Vodacom, USAID, Vodafone Foundation, Pathfinder International* na *Touch Foundation*. Mfumo huu unalenga kusaidia upatikanaji wa usafiri wa dharura kwa mama mjamzito, mama aliyejifungua na mtoto mchanga kote nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya mfumo kwa haraka na kwa kuwafikia walengwa wengi zaidi, kuna haja ya wadau mbalimbali kuongeza nguvu kwa kushirikiana katika utekelezaji wakiwemo watoa huduma wengine wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwaalika mashirika binafsi wakiwemo watoa huduma wengine wa mawasiliano pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo wajitokeze kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa Mfumo wa M-mama hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Kirumba, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, huduma hii tangu izinduliwe ni mwaka mmoja sasa na Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kampuni nyingine kuweza kujiunga kutoa huduma hii ya usafiri wa dharura kwa mama mjamzito na watoto.

Nini kauli ya Serikali kukamilisha mchakato huu kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kutokana na huduma hii kupatikana hasa maeneo ya mjini; je, Serikali imejipangaje kutoa elimu na matangazo ya kutosha kwa maeneo ya vijijini kuhusu huduma hii ya bure ya usafiri wa dharura wa mama mjamzito na mtoto? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Santiel, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba huduma hii toka imezinduliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni

karibia mwaka sasa, na maagizo yake yalikuwa mawili; moja, kuhakikisha tunapeleka nchi nzima. Hivi tunavyoongea, tumeshapeleka nchi nzima kasoro mikoa mitatu na kufikia tarehe 22/9/2023 tutakuwa tumewasha nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, la pili, lilikuwa hili la kutoa wito kwa wadau wengine kuendelea kuungana na Serikali katika kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi. Wadau wameendelea na mazungumzo na Serikali lakini waliopo wameendelea kuongeza fedha na ndiyo ambayo imetupa uwezo wa kuendelea kusambaza huduma hii maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kwamba huduma hii ni ngeni kwa baadhi ya maeneo na kwa hiyo, kutambulika kwake hakuwezi kwenda kwa mara moja. Tunachokifanya, kila tukipeleka mahali, tunaanza kutoa elimu kwa watendaji na hasa wale wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, huduma hii inasimamiwa kwa pamoja kati yetu Wizara ya Habari kama watoa teknolojia lakini Wizara ya Afya na TAMISEMI ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri, na idadi inaendelea kuongezeka siku hadi siku. Tunaamini tukishirikiana na Waheshimiwa Wabunge na hasa Wabunge wa Viti Maalum kupeleka hii elimu kwenye maeneo yetu ili akina mama watumie huduma hii kuokoa maisha ya mama na mtoto, itasaidia uelewa lakini pia itaongeza watumiaji wa huduma hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naishukuru Serikali kwa jitihada zake ambazo inazifanya kuhakikisha huduma hii imefika mijini. Swali langu ni kwamba: Je, ni upi mkakati wa kutoa elimu ya kutosha kwa akina mama hasa walioko vijijini ili waweze kujua nini maana ya huduma ya M-mama ili kupunguza vifo vya mama na mtoto hasa kwa maeneo ya vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza lengo la huduma hii kwa kweli siyo mijini sana, kwa sababu mijini huduma ziko karibu na watu. Lengo letu ni kupeleka vijijini ambako tatizo la upatikanaji wa huduma ni kubwa na hasa pale mama mjamzito au mtoto mchanga anapokosa huduma ya ziada baada ya kusaidiwa kwenye zahanati. Kwa hiyo, lengo letu ni kuwafikia walioko vijijini. Tukipeleka kwenye mkoa, tunataka iende vijijini ambako ndiko mahitaji yalipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu, lakini kama nilivyosema wakati najibu maswali ya nyongeza, nawaomba Wabunge wa Viti Maalum, tushirikiane tuzungumze tuone namna ya kuifikisha elimu hii kwa akina mama kwenye maeneo yetu ili waweze kuitumia huduma hii kwa sababu ipo, ni bure na inapatikana masaa 24 na inaokoa maisha ya mama na mtoto. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, swali la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Na. 20 la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, nimeletewa taarifa hapa kwamba ameliondoa kwa hivyo halitajibiwa na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea, Wabunge wanaotembea watafute mahali wakae. Naleta matangazo niliyonayo hapa. Ninalo tangazo la wageni.

Waheshimiwa Wabunge wanaozungumza wanisikilize.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mrisho Gambo ambaye ni mfanyabiashara kutoka China, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Asia Halamga ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Hanang. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wapiga kura wake kutoka Vwawa Mkoani Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mbulu, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza kinachofuata hapa ni majina. Mheshimiwa Tabasam, umenisikia? Utulivu kidogo, nazungumza na nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 52 wa Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Rehema tusikilizane.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wageni 62 ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi, na hawa ni kikundi cha mtandao wa *WhatsApp* kutoka Wilaya ya Babati Mjini, Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 70 kutoka Shule ya Msingi ya Awali *Peace and Love* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaye mwananchi mmoja kutoka Ubungo Dar es Salaam, Ndugu John Mpepo, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni. Kama wataendelea kuja wengine tutaendelea kuwatangaza ili mfahamu wapo hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, leo ni siku yetu ya kwanza ya Mkutano wetu huu wa Kumi na Mbili ambapo nataka kusema mambo machache ili tunapoendelea mbele tuwe wote tumeelewana sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, tulienda majimboni, tumewasikia wananchi wenzetu, na pia tumewasikia hata wale ambao siyo wa majimbo yetu wakiendelea kutoa maoni juu ya mambo mbalimbali ambayo yanaendelea hapa nchini. Sasa, kwa sababu sisi kama Wabunge, ni wawakilishi wa wananchi, tunawasikiliza wananchi mawazo yao, tunayachakata, tunaishauri Serikali. Yale ambayo tunapaswa kuisimamia Serikali, basi tunaisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mpina, siku nyingine ukiwa nje, ukisikia Spika anazungumza, unakaa nje unasubiri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa mawazo hayo yametolewa katika mawanda mapana sana; mapana sana kwa maana ya kwamba yamezungumziwa kwanza mambo mengi, na mengine mawazo hayo yalikuwa ni mambo mahususi; sasa yote ni kazi yetu kuyachukua, kuyafanyia kazi, kuishauri Serikali na yale ambayo tunapaswa kuisimamia Serikali, kuendelea kuisimamia Serikali.

Sasa ili tusiwe tunaenda mbele, tunarejea nyuma, kwa jambo mahususi linalohusu uwekezaji Bandarini, mawazo yaliyoendelea kutolewa na wananchi, baada ya Bunge kuwa limefanya maamuzi mwezi wa sita, sisi kama Wabunge ni kazi yetu kuendelea kuwasikiliza wananchi ili mawazo yao wakati utakapofika wa kuyatumia, tuyatumie hayo kuendelea kuishauri Serikali na wakati utakapofika wa kuisimamia Serikali, tutatumia mawazo hayo kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Katika upana wa mawanda wa mawazo yaliyotolewa, Bunge hili kwa sehemu, tulishamaliza kazi yetu. Kazi itakayofuata baada ya hapo, ni ya kuisimamia Serikali kwenye jambo ambalo Bunge lilishafanya maamuzi. Kwa hiyo, kwa kuwa Bunge lilishafanya maamuzi, tusije tukajikuta katika Bunge letu hili

tunarejea tena kwenye kutoa mawazo juu ya jambo hili hili ambalo tulishafanya maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wetu wa kuzungumza tena juu ya jambo hili kwa sababu, tulishafanya maamuzi, ni pale ambapo sheria inatupa nafasi nyingine. Hoja tukitaka Serikali ilete mikataba hapa Bungeni kuijadili, hoja itakuwa mbele yetu, na kwa hiyo, mawazo tunayoendelea kuyasikia kutoka kwa wananchi, wakati huo tutaweza kuyasema na kuiambia Serikali nini inapaswa kufanya kwa sababu tutafanya tena maamuzi mengine yatakayokuwa yanahusu hoja iliyopo mezani.

Nasema hivi ili tusije tukajikuta kwa sababu mawanda yaliyotolewa hayo maoni ni mapana sana, tusije tukajikuta na sisi tunakuja humu Bungeni, kutaka kufikiri tunaweza kutumia nafasi hii pengine kutoa ufafanuzi wa yale waliyoyasema ama wakati mwingne kutoa majibu juu ya hoja walizozitoa.

Sisi tulishafanya maamuzi na kama Wabunge ni kazi yetu kuendelea kuwasikiliza wananchi na kama Bunge ni kazi yetu kuendelea kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Utakapofika wakati wa kuisimamia Serikali sisi tutafanya kazi yetu na wananchi niwatoe wasiwasi wasiwe na wasiwasi juu ya jambo hilo.

Tutakapotaka kujua mikataba inayoingiwa na Serikali inasema nini, sheria zetu tulizozitunga zinaturuhusu tutaita mikataba hiyo na wananchi tutawafanyia kazi ile ambayo wametutuma kufanya hapa Bungeni ya kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sehemu nafikiri nitakuwa nimeeleweka hatutatumia Bunge hili kutoa ufafanuzi ama kujibu hoja za wananchi, ni kazi yetu kuzipokea hoja hizo, ni kazi yetu kupokea maoni yao na pale tunapoona upo ulazima basi Bunge litaleta hoja hizo hapa mezani na tutaweza kuzijadili kwa pamoja na kufanya maamuzi kama Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa mwelekeo huo wa jumla juu ya yale tuliyoyapokea kutoka majimboni na yale

ambayo yanaendelea kutolewa na wananchi basi tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU- KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitumie fursa hii kumuita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aje awasilishe hoja yake na Bunge tuweze kufanya kazi yetu. Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Feleshi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu, kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Bill, of 2023)*.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (*ndc.*) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, natoa pole za dhati kwa Bunge lako tukufu kwa kifo cha Mheshimiwa Francis Leonard Mtega Mbunge aliyefariki dunia tarehe 1 Julai, 2023. Natoa pole pia kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na hasa wananchi wa Mbarali kwa kumpoteza kiongozi ambaye alikuwa akiwatumikia.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Emanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bwana Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza, kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali kupitia wadau wote waliohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 *(The Atomic Energy Act, Cap.* 188);

(ii) Sheria ya Chuo cha Usafiri wa Majini Dar-es-Salaam, Sura ya 253 *(The Dar-es-Salaam Maritime Institute Act, Cap. 253);*

(iii) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, Cap. 449);*

(iv) Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, Cap. 450);*

(v) Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Sura ya 159 *(The Tanzania Industrial Research and Development Organisation Act, Cap. 159).*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu sita. Sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 ambapo kifungu cha 4 kinarekebishwa ili kuongeza mawanda ya udhibiti kwa kushusha viwango vya vyanzo mbalimbali vya mionzi vinavyosimamiwa na Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti mmuliko wa mionzi unaotokana na madini na Viasili vya Mionzi ya Asili *(NORMs)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya yanalenga kuweka masharti yanayozingatia viwango vya usalama vinavyokubalika Kimataifa. Vile vile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuruhusu utoaji wa misamaha ya viwango vya mionzi vinavyosimamiwa chini ya Sheria hii kwa kuzingatia vigezo na masharti yatakayoainishwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa lengo la kuongeza wigo wa udhibiti wa vyanzo vya mionzi ionishi *(ionizing radiation sources)*. Vilevile, kifungu kidogo cha (2) kinaongezwa kwa kuweka katazo la kushugulikia madini yanayotoa mionzi bila ya kuwa na leseni au kusajiliwa kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ulinzi na usalama katika kushughulika na vyanzo vya mionzi. Vifungu vya 20 na 24 vinapendekezwa kurekebishwa ili kudhibiti aina zote za vifaa vya mionzi ionishi vinavyohamishika. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa kudhibiti vifaa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 20A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka utaratibu wa utoaji vibali kwa watoa huduma za kitaalamu chini ya Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti huduma zinazotolewa ili kuhakikisha usalama katika utoaji wa huduma hizo. Kifungu cha 21 kinapendekezwa

kurekebishwa ili kushusha kiwango cha msamaha wakati wa usajili na utoaji leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ulinzi na usalama kwa wafanyakazi, umma na mazingira kutokana na mmuliko wa mionzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) ili kuweka sharti linaloelekeza cheti cha uchunguzi wa mionzi kitolewe kwa mnyororo wa chakula na bidhaa nyinginezo badala ya kutolewa kwa bidhaa za vyakula pekee kama ilivyo hivi sasa. Kifungu kidogo cha (2) kinaongezwa ili kuondoa ulazima wa kupata cheti cha uchunguzi wa mionzi iwapo bidhaa inayoingizwa nchini ina cheti kinachotambulika. Vilevile, kifungu kidogo cha (3) kinarekebishwa kwa kuweka utaratibu wa kufanya uchunguzi wa mnyororo wa chakula na bidhaa zinazotumika kwa ajili ya utafiti, usalama na ulinzi zinazoingizwa nchini au zinazosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 39 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ili kuweka masharti ya ulinzi dhidi ya uhalifu ikiwemo wizi, umiliki usio halali, usafirishaji haramu na uhujumu katika maeneo yanayohusika na nyuklia na viasili vya mionzi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ulinzi wa nyuklia na viasili vya mionzi dhidi ya matendo maovu. Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kudhibiti Viasili vya Mionzi ya Asili *(NORMs)* ambavyo havidhibitiwi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 58 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiondolea Bodi jukumu la ukaguzi wa mionzi na kulihamishia kwa Mkurugenzi Mkuu. Kifungu cha 72 kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) ili kuiondolea Tume mamlaka ya utozaji wa faini kwa mtu anayekiuka masharti ya Sheria. Inapendekezwa kuongeza kifungu cha 72A ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kufifilisha makosa. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama na kuongeza utii wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Chuo cha Usafiri

wa Majini Dar-es-Salaam, Sura ya 253 ambapo Sheria inafanyiwa marekebisho ya jumla ili kuainisha cheo sahihi cha Mkuu wa Taasisi hiyo kwa kuzingatia matakwa mapya ya *NACTVET*. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri za misamiati mbalimbali iliyotumika kwenye Sheria hii. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha majukumu ya Chuo yanayohusu usimamizi wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Bodi mamlaka ya kuunda kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake. Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiongezea Bodi mamlaka na majukumu yanayohusu utungaji wa sera, usimamizi na uidhinishaji wa hati za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 6A na 6B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uanzishwaji wa Baraza la Taaluma na majukumu yake kwa kuzingatia matakwa na viwango vya *NACTVET.* Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 7 ili kuongeza sharti linaloitaka Bodi kushauriana na Waziri wakati wa kutunga kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kutofautisha utaratibu wa utungaji wa kanuni kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Chuo ambazo hazina mahitaji ya kisera na utaratibu wa utungaji wa kanuni ambao unahusu masuala ya kisera.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha muda wa Mkuu wa Chuo kukaa madarakani ambapo inapendekezwa iwe kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuhamisha mamlaka ya kuidhinisha muundo wa chama cha wanafunzi kutoka kwa Waziri kwenda kwa Bodi ya Chuo. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na matakwa ya utendaji wa taasisi za elimu ambapo Bodi ndiyo inayohusika na uanzishwaji wa vyama vya wanafunzi badala ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, kichwa cha habari katika Sehemu ya Sita ya Sheria kinarekebishwa kwa kuondoa maneno *"Board of Examiners"* na badala yake kuweka neno *"Certification"*. Lengo la

marekebisho haya ni kuhuisha Sheria ili kuendana na utaratibu unaotumika sasa ambapo Bodi ya Watahini inasimamiwa na *TASAC*. Aidha, kifungu cha 11 kinarekebishwa ili kuweka sharti kwa wanafunzi wasio Watanzania kufanya malipo kwa kutumia fedha za kigeni kama itakavyoelekezwa na Chuo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa programu za mitihani zenye ithibati. Kifungu cha 13 kinachohusu Bodi ya Mitihani kinapendekezwa kufutwa ili majukumu yake yasimamiwe na Baraza la Taaluma kwa mujibu wa vifungu vya 6A na 6B. Kifungu cha 21 kinachohusu posho na ada za wajumbe wa Bodi kinapendekezwa kurekebishwa ili kiendane na Waraka wa Msajili wa Hazina unaotoa mwongozo wa masuala yanayohusu posho, ada na gharama za wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 22 kinachohusu Bodi kukasimu madaraka kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa hitaji la kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali hati za kukasimu madaraka ya Bodi. Kifungu cha 24 kinachoainisha mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha maeneo mbalimbali ambayo Waziri anaweza kuyatungia kanuni.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha vigezo vya kuzingatia wakati wa uteuzi wa wajumbe wa Bodi kuweka masharti kuhusu uendeshaji wa vikao na kuweka ukomo wa muda wa wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha Jedwali hilo na maelekezo ya Msajili wa Hazina kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa Vikao vya Bodi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne na Tano ya Muswada zinapendekeza maboresho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari, bandari za nchi kavu na bandari za maeneo ya maziwa nchini. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha bandari katika Jamhuri ya

Muungano kufikia viwango vya kimataifa vya kiutendaji na kuvutia nchi nyingi zaidi na shehena kubwa za mizigo kutumia bandari za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya majadiliano na Kamati kuhusu marekebisho ambayo yamependekezwa katika sehemu ya nne na tano na kukubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuondoa marekebisho hayo. Ili kutekeleza ushauri huo wa Kamati, Muswada umefanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho kwa kuondoa sehemu ya nne na tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Sura ya 159. Kifungu cha 4 kinachobainisha majukumu ya Shirika kinapendekezwa kurekebishwa ili kuliwezesha Shirika kufanya shughuli ambazo zinaendana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu uliopo na unaoendelea kutokea duniani.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha saba kinapendekezwa kurekebishwa ili kulipatia shirika mamlaka ya kuanzisha kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake. Kifungu cha nane kinachohusu uwasilishaji wa taarifa kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa masharti yake yamejumuishwa katika kifungu cha tisa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 kinachohusu uratibu wa tafiti zinazofanywa nje ya nchi kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa mfumo wa uchumi wa sasa umebadilika na shughuli za utafiti wa viwanda hazisimamiwi na Serikali pekee. Kifungu cha 13 kinachohusu mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti linalohusiana na maombi ya ufadhili wa tafiti za shirika nje ya nchi kwa kuwa utaratibu huo kwasasa hautumiki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 18 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza chanzo kipya cha mapato ili kuliwezesha shirika kupata fedha zinazotokana na michango na misaada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuziwezesha Mahakama zenye mamlaka kwenye maeneo husika kusikiliza mashauri yanayotokana na madai yanayohusu ushuru wa bidhaa za viwandani unaotozwa kwa mujibu wa kifungu hiki. Lengo la marekebisho haya ni kuziwezesha Mahakama hizo kusikiliza mashauri tofauti na utaratibu wa sasa ambapo mamlaka hayo yapo chini ya Mahakama za Hakimu Mkazi pekee.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 24 kinachohusu masuala ya ukaguzi wa fedha kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na masharti ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Jedwali la sheria linapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza wajumbe wa baraza ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2023]* kama ulivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (Na. 2) WA MWAKA 2023 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (No. 2) BILL, 2023) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2023).

**Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, ninawapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (*ndc.*) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji).

**Mheshimiwa Spika**, natoa pole za dhati kwa Bunge lako tukufu kwa kifo cha Mhe. Francis Leonard Mtega (Mb) aliyefariki dunia tarehe 1 Julai, 2023. Natoa pole pia kwa familia, ndugu, jamaa,

marafiki na hasa wananchi wa Mbarali kwa kumpoteza kiongozi ambaye alikuwa akiwatumikia.

**Mheshimiwa Spika**, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Emanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bw. Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza, kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali kupitia wadau wote waliohusika na sheria zinazopendekezwa kurekebishwa imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria zifuatazo:

(i) Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 (The Atomic Energy Act, Cap. 188);

(ii) Sheria ya Chuo cha Usafiri wa Majini Dar-es-Salaam, Sura ya 253 (The Dar-es-Salaam Maritime Institute Act, Cap. 253);

(iii) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 (The Natural Wealth and

Resources (Permanent Sovereignty) Act, Cap. 449);

(iv) Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 (The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, Cap. 450);

(v) Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Sura ya 159 (The Tanzania Industrial Research and Development Organisation Act, Cap. 159).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Sita. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 ambapo kifungu cha 4 kinarekebishwa ili kuongeza mawanda ya udhibiti kwa kushusha viwango vya vyanzo mbalimbali vya mionzi vinavyosimamiwa na Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti mmuliko wa mionzi unaotokana na madini na Viasili vya Mionzi ya Asili (NORMs). Aidha, marekebisho haya yanalenga kuweka masharti yanayozingatia viwango vya usalama vinavyokubalika Kimataifa. Vile vile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuruhusu utoaji wa misamaha ya viwango vya mionzi vinavyosimamiwa chini ya Sheria hii kwa kuzingatia vigezo na masharti yatakayoainishwa na Waziri.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa lengo la kuongeza wigo wa udhibiti wa vyanzo vya mionzi ionishi (ionizing radiation sources). Vile vile, kifungu kidogo cha (2) kinaongezwa kwa kuweka katazo la kushugulikia madini yanayotoa mionzi bila ya kuwa na leseni au kusajiliwa kwa madhumuni hayo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ulinzi na usalama katika kushughulika na vyanzo vya mionzi. Vifungu vya 20 na 24 vinapendekezwa kurekebishwa ili kudhibiti aina zote za vifaa vya mionzi ionishi vinavyohamishika.

Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa kudhibiti vifaa chini ya sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 20A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka utaratibu wa utoaji vibali kwa watoa huduma za kitaalamu chini ya Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti huduma zinazotolewa ili kuhakikisha usalama katika utoaji wa huduma hizo.

Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa ili kushusha kiwango cha msamaha wakati wa usajili na utoaji leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ulinzi na usalama kwa wafanyakazi, umma na mazingira kutokana na mmuliko wa mionzi.

Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) ili kuweka sharti linaloelekeza cheti cha uchunguzi wa mionzi kitolewe kwa mnyororo wa chakula na bidhaa nyinginezo badala ya kutolewa kwa bidhaa za vyakula pekee kama ilivyo hivi sasa. Kifungu kidogo cha (2) kinaongezwa ili kuondoa ulazima wa kupata cheti cha uchunguzi wa mionzi iwapo bidhaa inayoingizwa nchini ina cheti kinachotambulika. Vile vile, kifungu kidogo cha (3) kinarekebishwa kwa kuweka utaratibu wa kufanya uchunguzi wa mnyororo wa chakula na bidhaa zinazotumika kwa ajili ya utafiti, usalama na ulinzi zinazoingizwa nchini au zinazosafirishwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 39 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ili kuweka masharti ya ulinzi dhidi ya uhalifu ikiwemo wizi, umiliki usio halali, usafirishaji haramu na uhujumu katika maeneo yanayohusika na nyuklia na viasili vya mionzi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ulinzi wa nyuklia na viasili vya mionzi dhidi ya matendo maovu. Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kudhibiti Viasili vya Mionzi ya Asili (NORMs) ambavyo havidhibitiwi kwa sasa.

Kifungu cha 58 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiondolea Bodi jukumu la ukaguzi wa mionzi na kulihamishia kwa Mkurugenzi Mkuu. Kifungu cha 72 kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo

cha (4) ili kuiondolea Tume mamlaka ya utozaji wa faini kwa mtu anayekiuka masharti ya Sheria. Inapendekezwa kuongeza kifungu cha 72A ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kufifilisha makosa. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama na kuongeza utii wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Chuo cha Usafiri wa Majini Dar-es-Salaam, Sura ya 253 ambapo Sheria inafanyiwa marekebisho ya jumla ili kuainisha cheo sahihi cha Mkuu wa Taasisi hiyo kwa kuzingatia matakwa mapya ya NACTVET. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha tafsiri za misamiati mbalimbali iliyotumika kwenye Sheria hii. Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha majukumu ya Chuo yanayohusu usimamizi wa mitihani.

Kifungu cha 5 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Bodi mamlaka ya kuunda kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake. Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuiongezea Bodi mamlaka na majukumu yanayohusu utungaji wa sera, usimamizi na uidhinishaji wa hati za kiutendaji.

Vifungu vya 6A na 6B vinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uanzishwaji wa Baraza la Taaluma na majukumu yake kwa kuzingatia matakwa na viwango vya NACTVET. Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 7 ili kuongeza sharti linaloitaka Bodi kushauriana na Waziri wakati wa kutunga kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kutofautisha utaratibu wa utungaji wa kanuni kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Chuo ambazo hazina mahitaji ya kisera na utaratibu wa utungaji wa kanuni ambao unahusu masuala ya kisera.

Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha muda wa Mkuu wa Chuo kukaa madarakani ambapo inapendekezwa iwe kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuhamisha mamlaka ya kuidhinisha muundo wa chama cha wanafunzi kutoka kwa Waziri kwenda kwa Bodi ya Chuo. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na matakwa ya

utendaji wa taasisi za elimu ambapo Bodi ndiyo inayohusika na uanzishwaji wa vyama vya wanafunzi badala ya Waziri. Kichwa cha Habari katika Sehemu ya Sita ya Sheria kinarekebishwa kwa kuondoa maneno "Board of Examiners" na badala yake kuweka neno "Certification". Lengo la marekebisho haya ni kuhuisha Sheria ili kuendana na utaratibu unaotumika sasa ambapo Bodi ya Watahini inasimamiwa na TASAC. Aidha, kifungu cha 11 kinarekebishwa ili kuweka sharti kwa wanafunzi wasio Watanzania kufanya malipo kwa kutumia fedha za kigeni kama itakavyoelekezwa na Chuo.

Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa programu za mitihani zenye ithibati. Kifungu cha 13 kinachohusu Bodi ya Mitihani kinapendekezwa kufutwa ili majukumu yake yasimamiwe na Baraza la Taaluma kwa mujibu wa vifungu vya 6A na 6B. Kifungu cha 21 kinachohusu posho na ada za wajumbe wa Bodi kinapendekezwa kurekebishwa ili kiendane na Waraka wa Msajili wa Hazina unaotoa mwongozo wa masuala yanayohusu posho, ada na gharama za wajumbe wa Bodi.

Kifungu cha 22 kinachohusu Bodi kukasimu madaraka kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa hitaji la kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali hati za kukasimu madaraka ya Bodi. Kifungu cha 24 kinachoainisha mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha maeneo mbalimbali ambayo Waziri anaweza kuyatungia kanuni.

Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha vigezo vya kuzingatia wakati wa uteuzi wa wajumbe wa Bodi kuweka masharti kuhusu uendeshaji wa vikao na kuweka ukomo wa muda wa wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha Jedwali hilo na maelekezo ya Msajili wa Hazina kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa Vikao vya Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne na Tano ya Muswada zinapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 ili kuhakikisha utekelezaji wa

Sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari, bandari za nchi kavu na bandari za maeneo ya maziwa nchini. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwezesha bandari katika Jamhuri ya Muungano kufikia viwango vya kimataifa vya kiutendaji na kuvutia nchi nyingi zaidi na shehena kubwa za mizigo kutumia bandari za hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya majadiliano na Kamati kuhusu marekebisho ambayo yamependekezwa katika Sehemu ya Nne na Tano na kukubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuondoa marekebisho hayo. Ili kutekeleza ushauri huo wa Kamati, Muswada umefanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho kwa kuondoa Sehemu ya Nne na Tano.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Sura ya 159. Kifungu cha 4 kinachobainisha majukumu ya Shirika kinapendekezwa kurekebishwa ili kuliwezesha Shirika kufanya shughuli ambazo zinaendana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu uliopo na unaoendelea kutokea duniani.

Kifungu cha 7 kinapendekezwa kurekebishwa ili kulipatia shirika mamlaka ya kuanzisha kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake. Kifungu cha 8 kinachohusu uwasilishaji wa taarifa kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa masharti yake yamejumuishwa katika kifungu cha 9.

Kifungu cha 12 kinachohusu uratibu wa tafiti zinazofanywa nje ya nchi kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa mfumo wa uchumi wa sasa umebadilika na shughuli za utafiti wa viwanda hazisimamiwi na Serikali pekee. Kifungu cha 13 kinachohusu mamlaka ya Waziri kutunga kanuni kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti linalohusiana na maombi ya ufadhili wa tafiti za Shirika nje ya nchi kwa kuwa utaratibu huo kwa sasa hautumiki.

Kifungu cha 18 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza chazo kipya cha mapato ili kuliwezesha Shirika kupata fedha zinazotokana na michango na misaada mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa

marekebisho ili kuziwezesha Mahakama zenye mamlaka kwenye maeneo husika kusikiliza mashauri yanayotokana na madai yanayohusu ushuru wa bidhaa za viwandani unaotozwa kwa mujibu wa kifungu hiki. Lengo la marekebisho haya ni kuziwezesha Mahakama hizo kusikiliza mashauri tofauti na utaratibu wa sasa ambapo mamlaka hayo yapo chini ya Mahakama za Hakimu Mkazi pekee.

Kifungu cha 24 kinachohusu masuala ya ukaguzi wa fedha kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na masharti ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Jedwali la Sheria linapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza wajumbe wa Baraza ili kupunguza gharama za uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 (the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2023) kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** NAOMBA KUTOA HOJA.

Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.)
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
29/08/2023

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama aje awasilishe maoni ya Kamati.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2023 *[The Written Laws Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2023]*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na moja, kikao cha hamsini na saba kwenye Bunge la 12, tarehe 28 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge uliuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na ujadiliwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati uliuchambua na kuujadili Muswada kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali 15 Agosti, 2023 ili kupata maelezo ya Mheshimiwa Dkt. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing)* tarehe 16 Agosti, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi

mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wadau wote waliojitokeza kwa madhumuni ya kuleta maoni yao ili kuboresha Muswada huu; na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. *The Tanganyika Law Society (TLS);*

2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC);*

3. Taasisi ya Haki Rasilimali;

4. Tanzania *Fishers (TAF);*

5. Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi;

6. Tanzania *Network of Legal Aid Providers (TANLAP)*; pamoja; na

7. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau katika sehemu ya kwanza, ya pili, ya tatu na sehemu ya sita. Mnamo tarehe 21 Agosti, 2023 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za muswada.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa muswada. Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2023 ukiwa umegawanyika katika sehemu kuu sita na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tano kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo: -

(a) Sheria ya Nguvu ya Atomu Sura ya 188 *(The Atomic Energy Act, (Cap. 188);*

(b) Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Sura ya 253 *(The Dar es Salaam Maritime Institute Act, (Cap. 253);*

(c) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 *[The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449)];*

(d) Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 *[The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiate of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)]; na*

(e) Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159 *[The Tanzania Industrial Research and Development Organization Act, (Cap 159)]*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya 1 ambayo inahusu jina fupi la Ibara na Ibara ya 2 inaeleza marekebisho yaliyofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa vifungu mbalimbali. Sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Nguvu ya Atomu Sura ya 188. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 15 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii kwa ujumla yanalenga kuharakisha utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama na kuongeza utii wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Sura ya 253. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 16 hadi Ibara ya 34 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu hii yanalenga pamoja na mambo mengine kuainisha cheo sahihi cha Mkuu wa Chuo hicho kwa kuzingatia matakwa mapya ya Baraza la Kitaifa

la Elimu ya Ufundi kama inavyofafanuliwa katika ibara ya 17 ya muswada huu.

Mheshimiwa Spika, vilevile ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2 cha Sheria kinachohusu tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kufuta neno *minister* na badala yake kuweka neno *board* katika tafsiri ya neno *student organisation*. Lengo la marekebisho hayo ni kumuondoa Waziri kutoa ithibati ya uendeshwaji wa chama cha wanafunzi na jukumu hilo kutekelezwa na bodi.

(b) Kuongeza tafsiri ya maneno *academic council* yakiwa na maana ya Baraza la Taaluma.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 6A na 6B mara baada ya Kifungu cha 6. Ufafanuzi wa vifungu hivyo ni kama ifuatavyo: -

Kifungu cha 6A kinalengo la kuanzisha Baraza la Taaluma la Chuo chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Chuo, akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia taaluma, utafiti na ushauri. Wajumbe wengine wanaounda baraza hilo ni

(i) Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala;

(ii) Wakuu wa Idara mbalimbali za Chuo;

(iii) Mkuu wa Kitengo cha Sheria;

(iv) Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ubora;

(v) Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

(vi) Mlezi wa Wanafunzi;

(vii) Msajili;

(viii) Wawakilishi wawili kutoka Chama cha Wanafunzi;

(ix) Wawakilishi wawili wanaowakilisha vyuo vingine vya Kitaaluma; na

(x) Wawakilishi wawili kutoka vyuo vingine vinavyohusu masuala ya bahari.

Mheshimiwa Spika, ibara ndogo ya pili (2) inaeleza kuwa muda wa Wajumbe wa Baraza kukaa madarakani ni miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine. Ibara ndogo ya tatu inalipatia baraza mamlaka ya kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao cha baraza na kutoa ushauri kwenye jambo mahsusi lakini mwalikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne na sehemu ya tano zinapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu umiliki wa mali na rasilimali asilia, sura ya 449 *[The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449)]* na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 *(The Natural Wealth and Resources [Review and Re-Negotiate Unconditioned Terms) Act, (Cap. 450)]*.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 36 na 38 ya Muswada huu unapendekeza marekebisho kwa kufuta kifungu cha 2 (2) cha sheria hizo mtawaliwa na kukiandika upya kwa lengo la kuondoa masharti ya sheria hizo zisitumike katika makubaliano yanayohusu usafirishaji wa rasilimali asilia ambazo hazijachumwa ndani ya nchi.

Aidha, marekebisho hayo yanakusudia kuondoa matumizi ya sheria hii kwenye masuala yanayohusu uendelezaji, uendeshaji au mpango wa uendelezaji wa utajiri wa mali za asili endapo kutakuwa na lengo la kuboresha utendaji/ufanisi wa bandari za bahari, bandari kavu na maziwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla maboresho hayo yanalenga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari, bandari za nchi kavu na bandari za maeneo ya maziwa nchini, ili kuwezesha bandari katika Jamhuri ya Muungano kufikia viwango vya kimataifa vya utendaji na kuvutia nchi nyingi zaidi na shehena kubwa za mizigo kutumia bandari za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159. Sehemu hii inahusu Ibara ya 39 hadi Ibara ya 49, ambapo Ibara ya 39 inaeleza kuwa sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania *(The Tanzania Industrial Research and Development Organization Act),* ambayo inajulikana kama sheria kuu.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 40 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4(1) cha sheria kama ifuatavyo: -

(i) Kufuta maneno *applied research* na badala yake kuweka maneno *industrial research.*

(ii) Kufuta aya (a) na kuiandika upya ili kulipatia Shirika jukumu la kufanya au kuhamasisha ufanyaji wa tafiti za viwanda.

(iii) Kufuta neno *local* katika aya (c), ili kuwezesha Shirika kutoa mafunzo kwa watu wote.

(iv) Kufuta aya (d) na kuiandika upya ili kulipatia Shirika jukumu la kufanya ufuatiliaji wa viwanda kwa lengo la kufanya tathmini ya utendaji na tija yake ili kuzuia hasara inayoweza kujitokeza.

(v) Kuongeza aya mpya (g) mara baada ya aya (f) ili kulipatia Shirika jukumu la kutoa ushauri wa kitalaam kuhusu uendelezaji wa viwanda.

(vi) Kurekebisha aya (g), (h) na (i) kuwa aya (h), (i) na (j) mtawalia;

(vii) Kufuta aya (j) iliyobadilishwa na kuandikwa upya ili kulipatia Shirika jukumu la kutoa ushauri katika uanzishaji wa mfumo wa udhibiti na kuratibu uchakataji viwandani ili kuboresha utendaji na kuzuia uchafuzi wa viwanda.

(viii) Kuongeza aya (k), (l) na (m) mara baada ya aya (j) ili kulipatia Shirika jukumu la kupima na kuchambua teknolojia za viwandani na mashine za kupima matokeo ya utafiti na uvumbuzi.

Aidha, ibara ya 41 ya muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 cha sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) mara baada ya Kifungu kidogo cha (4). Lengo ni kuliwezesha baraza kuanzisha kamati mbalimbali kadri itakavyoonekana ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mapendekezo katika sehemu hii yanalenga kuboresha majukumu ya shirika ili kuruhusu shirika kufanya shughuli zake ambazo zinaendana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu uliopo na unaoendelea kutokea duniani kote. Pia, majukumu hayo yanarekebishwa ili kuondoa mgongano kati ya majukumu ya shirika na majukumu ya taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam. Katika Ibara ya 22 Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kipya cha 6(a) kwenye sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam ili kuunda Baraza la Taaluma la Chuo. Kamati ilishauri ukubwa wa baraza hilo upunguzwe kwa kuwa linaonekana linaundwa na idadi kubwa ya wajumbe. Vilevile kamati ilishauri idara zinazohusika na taaluma moja kwa moja

ndizo ziunde baraza, ukizingatia kuwa baraza linapendekeza kuunda kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Katika Ibara ya 27(b) Kamati ilipendekeza kutokuandika *Us Dollars* kama mfumo rasmi wa malipo ya ada ya wanafunzi wasio Watanzania na badala yake sheria itambue fedha za kigeni zote ambazo zinaweza kubadilishwa hapa Tanzania *(convertible currencies)*. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 34 ya Muswada, kamati ilipendekeza kurekebisha Jedwali la Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam kwa kufuta aya ya 7 na kuandika upya ili kumuwezesha Mwenyekiti au Makamu wake kuitisha kikao maalum cha baraza *(council)* baada ya kupokea maombi ya idadi kubwa ya wajumbe. Kwa kuwa jedwali linahusu vikao vya bodi, kamati ilipendekeza neno *council* liondolewe na badala yake liwekwe neno *board* ili kuendana na malengo ya jedwali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubalina na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Mamlaka ya Nchi, kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano, kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450. Katika Ibara 35 hadi 38 ya Muswada, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu maudhui ya marekebisho hayo. Baada ya majadiliano hayo Serikali ilikubali ushauri wa Kamati na kuleta marekebisho kwa kufuta Sehemu ya Nne na Tano ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159. Ibara ya 43(b) ya Muswada inapendekeza kuweka adhabu kuhusu makosa yanayotokana na kukiuka sheria ya Shirika la Utafiti wa Viwanda *(TIRDO)* kwa kufuta maneno "*not exceeding fifteen thousand shillings*" na kuweka maneno "*not less than fifty thousand shillings but not exceeding five million shillings*".

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri marekebisho kwa kuwa mapendekezo hayo yana tofauti kubwa kati ya adhabu ya chini na adhabu ya juu. Hali hii inaweza kupelekea matumizi mabaya ya mamlaka ya kutoza faini. Kamati ilipendekeza adhabu ziwekwe kulingana na uzito wa makosa, ambapo makosa madogo yawe na adhabu zake maalum kulingana na udogo wake na makosa makubwa yawe na adhabu zake kulingana na uzito wa kosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri huo wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu, ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yaliyopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria; Mheshimiwa Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Ndugu Onorius Njole; pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu na kushughulikia shughuli hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 2 WA MWAKA 2023 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.2) BILL, 2023]* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na. 2 wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na moja, kikao cha hamsini na saba kwenye Bunge la 12, tarehe 28 Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati iliuchambua na kuujadili Muswada kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 15 Agosti, 2023 ili kupata maelezo ya Mhe. Jaji

Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* tarehe 16 Agosti, 2023 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. The Tanganyika Law Society (*TLS*)
2. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*)
3. Taasisi ya Haki Rasilimali
4. Tanzania Fishers (*TAF*)
5. Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi
6. Tanzania Network of Legal Aid Providers (*TANLAP*); pamoja na
7. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau katika sehemu ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya sita. Mnamo tarehe 21 Agosti, 2023 Kamati ilikutana tena na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2023 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023]* ukiwa umegawanyika katika sehemu kuu sita (6) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tano (5) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Nguvu ya Atomu Sura ya 188 (*The Atomic Energy Act, (Cap. 188);*

(b) Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Sura ya 253 *(The Dar es Salaam Maritime Institute Act, (Cap. 253)*;

(c) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449*);

(d) Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 (*The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiate of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)*; na

(e) Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159 *(The Tanzania Industrial Research and Development Organization Act, (Cap 159)*.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina fupi na

**Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Nguvu ya Atomu Sura ya 188 (*The Atomic Energy Act, (Cap. 188)***. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 15 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii kwa ujumla yanalenga kuharakisha utatuzi wa migogoro nje ya Mahakama na kuongeza utii wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Sura ya 253 *(The Dar es Salaam Maritime Institute Act, (Cap. 253)***. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 16 hadi Ibara ya 34 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu hii yanalenga pamoja na mambo mengine kuainisha cheo sahihi cha Mkuu wa Chuo hicho kwa kuzingatia matakwa mapya ya Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (***NACTVET***) kama inavyofafanuliwa katika Ibara ya 17 ya Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile Ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2 cha Sheria kinachohusu tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kufuta neno "*Minister*" na badala yake kuweka neno "*Board*" katika tafsiri ya neno "*student organisation*". Lengo la marekebisho haya ni kumuondoa Waziri kutoa ithibati ya uanzishwaji wa chama cha wanafunzi na jukumu hilo kutekelezwa na Bodi.

(b) Kuongeza tafsiri ya maneno "*Academic Council*" yakiwa na maana ya Baraza la Taaluma.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 6A na 6B mara baada ya Kifungu cha 6. Ufafanuzi wa vifungu hivyo ni kama ifuatavyo: -

Kifungu cha 6A kinalengo la kuanzisha Baraza la Taaluma la Chuo chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Chuo, akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri. Wajumbe wengine wanaounda Baraza hilo ni:-

(i) Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala;

(ii) Wakuu wa Idara mbalimbali za Chuo;

(iii) Mkuu wa Kitengo cha Sheria;

(iv) Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ubora;

(v) Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

(vi) Mlezi wa Wanafunzi;

(vii) Msajili;

(viii) Wawakilishi wawili kutoka Chama cha Wanafunzi;

(ix) Wawakilishi wawili wanaowakilisha vyuo vingine vya Kitaaluma; na

(x) Wawakilishi wawili kutoka vyuo vingine vinavyohusu masuala ya bahari.

Ibara ndogo ya (2) inaeleza kuwa muda wa wajumbe wa Baraza kukaa madarakani ni miaka mitatu, na wanaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine. Ibara ndogo ya (3) inalipatia Baraza mamlaka ya kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao cha Baraza na kutoa ushauri kwenye jambo mahsusi lakini mwalikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne na Sehemu ya Tano zinapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap.***

***449*)** na **Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 (*The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiate of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)*.**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 36 na 38 ya Muswada huu unapendekeza marekebisho kwa kufuta kifungu cha 2(2) cha sheria hizo mtawalia na kukiandika upya kwa lengo la kuondoa masharti ya sheria hizo zisitumike katika makubaliano yanayohusu usafirishaji wa Rasilimali Asilia ambazo hazijachumwa *(not exploited)* nchini.

Aidha, marekebisho hayo yanakusudia kuondoa matumizi ya sheria hii kwenye masuala yanayohusu uendelezaji, uendeshaji au mpango wa uendelezaji wa utajiri wa mali za asili endapo kutakuwa na lengo la kuboresha utendaji/ufanisi wa bandari za bahari, bandari kavu na maziwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla maboresho haya yanalenga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari, bandari za nchi kavu na bandari za maeneo ya maziwa nchini, ili kuwezesha bandari katika Jamhuri ya Muungano zinafikia viwango vya kimataifa vya utendaji na kuvutia nchi nyingi zaidi na shehena kubwa za mizigo kutumia bandari za hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159 *(The Tanzania Industrial Research and Development Organizsation Act, (Cap 159)*.**

Sehemu hii inahusu ibara ya 39 hadi 49 ambapo Ibara ya 39 inaeleza kuwa, sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, yani *the Tanzania Industrial Research and Development Organization Act*, ambayo inajulikana kama sheria Kuu (*The Principal Act*).

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 40 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4(1) cha sheria kama ifuatavyo: -

(i) kufuta maneno "*applied research*" na badala yake kuweka maneno "*industrial research*".

(ii) kufuta aya (a) na kuiandika upya ili kulipatia Shirika jukumu la kufanya au kuhamasisha ufanyaji wa tafiti za viwanda.

(iii) kufuta neno "*local*" katika aya (c), ili kuwezesha Shirika kutoa mafunzo kwa watu wote.

(iv) kufuta aya (d) na kuiandika upya ili kulipatia Shirika jukumu la kufanya ufuatiliaji wa viwanda kwa lengo la kufanya tathmini ya utendaji na tija yake ili kuzuia hasara inayoweza kujitokeza.

(v) Kuongeza aya mpya (g) mara baada ya aya (f) ili kulipatia Shirika jukumu la kutoa ushauri wa kitalaam kuhusu uendelezaji wa viwanda.

(vi) kurekebisha aya (g), (h) na (i) kuwa aya (h), (i) na (j) mtawalia;

(vii) kufuta aya (j) iliyobadilishwa na kuiandika upya ili kulipatia Shirika jukumu la kutoa ushauri katika uanzishaji wa mfumo wa kudhibiti na kuratibu uchakataji viwandani ili kuboresha utendaji na kuzuia uchafuzi wa viwanda.

(viii) kuongeza aya (k), (l) na (m) mara baada ya aya (j) ili kulipatia Shirika jukumu la kupima na kuchambua teknolojia za viwandani na mashine za kupima matokeo ya tafiti na uvumbuzi.

Aidha, Ibara ya 41 ya muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 cha sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) mara baada ya Kifungu kidogo cha (4). Lengo ni kuliwezesha Baraza kuanzisha kamati mbalimbali kadri itakavyoonekana ni muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla mapendekezo katika sehemu hii yanalenga kuboresha majukumu ya Shirika ili kuruhusu Shirika kufanya shughuli zake ambazo zinaendana na maendeleo ya

sayansi, teknolojia na ubunifu uliopo na unaoendelea kutokea Duniani kote. Pia, majukumu hayo yanarekebishwa ili kuondoa mgongano kati ya majukumu ya Shirika na majukumu ya Taasisi nyingine.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, SURA ya 253 (*The Dar Es Salaam Maritime Institute ACT, CAP.253)*

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 22 Kamati ilipendekeza kuongeza kifungu kipya cha 6A kwenye sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam ili kuunda Baraza la Taaluma la Chuo. Kamati ilishauri ukubwa wa Baraza hilo upunguzwe kwa kuwa linaonekana linaundwa na idadi kubwa ya wajumbe. Vilevile, Kamati ilishauri idara zinazohusika na taaluma moja kwa moja ndio ziunde Baraza, ikizingatiwa kuwa Baraza linapendekeza kuunda kamati mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Baraza la Taaluma la chuo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 27(b) Kamati ilipendekeza kutokuandika "*Us Dollars*" kama mfumo rasmi wa malipo ya ada ya wanafunzi wasio watanzania na badala yake sheria itambue fedha za kigeni zote ambazo zinaweza kubadilishwa hapa Tanzania "*convertible currency*".

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kutambua fedha za kigeni zote ambazo zinaweza kubadilishwa hapa Tanzania kama malipo ya ada kwa wanafunzi wasio Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 34 ya Muswada Kamati ilipendekeza kurekebisha Jedwali la sheria ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam kwa kufuta aya ya 7 na kuiandika upya ili kumuwezesha Mwenyekiti au Makamu wake kuitisha kikao maalum cha Baraza (*council*) baada ya kupokea maombi ya idadi kubwa ya wajumbe. Kwa kuwa jedwali linahusu vikao vya Bodi, Kamati ilipendekeza neno "*council*" liondolewe na badala yake liwekwe neno "*board*" ili kuendana na malengo ya Jedwali.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kutumia neno *board* badala ya *council* ili kuendana na malengo ya jedwali husika.

**3.3 Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449*)** na **Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450 (*The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiate of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)*.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Ibara 35 hadi 38 ya Muswada, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali kuhusu maaudhui ya marekebisho hayo. Baada ya majadiliano hayo Serikali ilikubali ushauri wa Kamati na kuleta marekebisho kwa kufuta Sehemu ya Nne na Tano ya Muswada.

### 3.4 Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Sura ya 159 *(The Tanzania Industrial Research and Development Organization Act, (Cap 159)*.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 43(b) ya Muswada inapendekeza kuweka adhabu kuhusu makosa yanayotokana na kukiuka sheria ya Shirika la Utafiti wa Viwanda *(TIRDO)* kwa kufuta maneno "*not exceeding fifteen thousand shillings*" na kuweka maneno "*not less than fifty thousand shillings but not exceeding five million shillings*". Kamati ilishauri maboresho kwa kuwa mapendekezo hayo yana tofauti kubwa kati ya adhabu ya chini na adhabu ya juu. Hali hii inaweza kupelekea matumizi mabaya ya madaraka ya kutoza faini. Kamati ilipendekeza adhabu ziwekwe kulingana na uzito wa kosa, ambapo makosa madogo yawe na adhabu zake maalum kulingana na udogo wake, na makosa makubwa yawe na adhabu zake kulingana na uzito wa kosa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufuata ushauri wa Kamati kwa kuweka adhabu kulingana na uzito wa kosa.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb – **M/Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe

8. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Damas Daniel Ndumbaro (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Philipo Gekul (Mb) Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mhe. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

29 Agosti, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ambayo imefanya kazi kwa niaba ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu ninayo majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wanatamani kuchangia mabadiliko haya ambayo yamependekezwa. Tutaanza na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa na Mheshimiwa Yahya Omary Massare ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nimpongeze Waziri wa Sheria na *Attorney General* na Kamati kwa wasilisho zuri linalohusu marekebisho ya Sheria Mbalimbali *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No.2) Bill, 2023)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Kamati Muswada huu unahusu sheria tano. Kwa kuanzia, nianze na Sehemu ya Tatu na ya Nne ya Muswada ambao ulikuwa unahusu sheria mbili za *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act* ambayo baada ya mashauriano na Ofisi ya *Attorney General* Serikali ilikuwa inataka kuibadilisha Kifungu cha 35, 36 na Ibara ya 37 na 38, lakini baada ya mashauriano na kuona mantiki, Serikali kupitia *Attorney General* waliomba ku–*withdraw*. Kwa kweli tuwapongeze hata wadau ambao walikuja mbele ya Kamati yetu, maoni yao mengi sana yalikuwa yanagusa sehemu ya hizi Sheria mbili, kwa hiyo tunawapongeza Serikali kwa busara hiyo kubwa kuhusu hizi sheria mbili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na sababu nyingi, kuna kesi zinazoendelea mahakamani lakini pia kuna kanuni zetu za Bunge zinazotuzuia kuzungumzia masuala ambayo yapo mahakamani. Pamoja na hayo yote tunaishukuru Serikali kwa kuondoa sehemu hizi mbili za Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ni *The Atomic Energy Act* na hapa niipongeze Wizara ya Elimu kupitia Tume ile ya *Tanzania Energy Commission,* walialika Kamati tutembelee Arusha na tuone kituo chetu cha *energy*. Sijui Wabunge wangapi

wanafahamu hii Tume ambayo inafanya kwa kweli kazi nzuri sana. Wanajaribu kuratibu haya masuala ya *atomic* na kwa kweli Wajumbe wa Kamati yetu waliotembelea, walijifunza mambo mengi sana. Madhara tunayopata kutokana na simu hizi, *microwave* na haya mambo yote ambayo yana *radioactive elements,* kwa kweli tulijifunza sana na tunaomba Tume hii iendelee kutoa elimu kwa Watanzania kupitia vyombo vya habari, ili waendelee kujifunza athari ambazo zinatokana na *the atomic energy*.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Kamati mabadiliko haya ni kuwezesha Tume kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Kwa mfano, kuna Kifungu cha 10 kinachozungumzia *The Atomic Energy Act.* Kwanza ukisoma Kifungu cha 4 utaona mabadiliko yake ni kupunguza kiasi cha mionzi kwenye vitu mbalimbali na hii ni kuendana pia na *obligations* za kimataifa. Tunajua nchi yetu ni sehemu ya dunia na kuna Shirika la Kimataifa linaloitwa *The International Atomic Agency,* ambalo lina–*regulate* mambo ya *atomic energy* na ili sasa tuondokane na jukumu hili na ambalo mara kwa mara huwa linatoa miongozo ya namna nchi ambazo ni wanachama wanufaike. Msingi wake ni kuhakikisha tu usalama wa wale ambao wanafanya kazi kwenye vyombo hivi na Watanzania kwa ujumla wanakuwa hawapati madhara ambao yanatokana na *radioactive elements.*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 11 utaona vile vile vitu ambavyo vilikuwa vinapatikana kwa mfano sheria inasema hivi, viwango ambavyo vilikuwa viko – *exempted* kuna kitu kinaitwa *becquerel. Becquerel* ni jina la kisayansi ilikuwa inasema kati ya 74 mpaka 3,700. Sasa kwa mabadiliko haya ni kupunguza sasa kiasi hicho ili kuipa Tume hii mamlaka ya kupata kazi kubwa zaidi ya kuweza kuondoa, kushughulika na vile vitu ambavyo vina hiyo mionzi kuanzia *becquerel* moja na kumi na hii itaongezea kazi kubwa Tume, lakini kusudi la haya yote ni kulinda afya za Watanzania. Kwa hiyo tuipongeze Serikali kwa kuliona hili ili kulinda afya za Watanzania wasipate maradhi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko mengine ya Sheria hii ya *Dar es Salaam Maritime Institute,* vilevile kutokana na mabadiliko ya Sheria iliyofanywa na Bunge hili 2021 kuna mabadiliko kutoka

*NACTE* sasa kwenda kwenye *Institute* nyingine ambayo imebadilika jina sasa inaitwa *The National Council for Technical Education* kwa kuongeza kitu kinachoitwa Technical *Vocational Educational Training.* Kwa hiyo mabadiliko hayo sasa yatawezesha Sheria hii na Chuo hiki kiendane sasa na mabadiliko ya sheria.

Mheshimiwa Spika, tukirudi vile vile kwenye *The Atomic Energy Act,* mtu alikuwa akikutwa na kosa kwa mfano, Tume hii ilikuwa na mamlaka ya kumpeleka huyu mtu mahakamani. Kwa hiyo kesi zinakuwa ni nyingi, lakini ilikuwa haina uwezo wa ku–*sanction* na kutoza *fine* wale ambao watakuwa wame–*violate* sheria. Kwa hiyo, mabadiliko hayo kama tutakavyoona kwenye kifungu cha 72 inaiwezesha Tume sasa kuwa na mamlaka mapana zaidi ya kuweza ku–*compound* kwa mtu ambaye atakuwa amekosea. Tume iwe na mamlaka hayo ya kutoza faini za haraka haraka bila kupeleka mahakamani. Hii itawezesha Tume kufanya kazi kwa wakati na bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, vilevile utaona mabadiliko ya Sheria hii ta *Tanzania Industrial Research* na hii pia ni kuendana na mabadiliko ya uchumi duniani. Sasa tunajua uchumi siyo *state controlling* peke yake, kuna *private sectors.* Kwa hiyo sharti la sheria hii kabla ilikuwa ni kujaribu kuleta *assumption* kwamba ni Serikali peke yake inahusika na mambo ya *industrial research,* kwa hiyo naipongeza Serikali kwa kuliona hili mapema kabla halijaonekana kwamba ni *barrier.*

Mheshimiwa Spika, kimsingi sheria zetu hizi zingine za 2003, zingine za 1992, kutokana na mabadiliko ambayo yanaendelea kwenye sekta mbalimbali sheria zetu ili tufanye sasa ziendane na *standards* na miongozo mipya ambayo nchi yetu inapitia.

Mheshimiwa Spika, sharti la kushtaki, sheria ilikuwa inasema Mkurugenzi anaweza akampeleka mtu kwa mahakama ya Hakimu Mkazi peke yake na tunafahamu siyo kila mahali tuna Mahakama hizi za Makimu Mkazi ama *Regional Magistrate.* Sasa kuondoa takwa hilo na kusema kwamba Mkurugenzi huyu awe na mamlaka ya kuweza kumshtaki mtu huyo popote kwenye mahakama, iwe ni Mahakama ya Mwanzo au mahakama yoyote

ambayo itakuwa kwenye eneo hilo. Nadhani itasaidia bodi hii kuwa *effective* zaidi na itafanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache sana, naipongeza Kamati kwa kufanya kazi nzuri sana na napongeza Serikali na naunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Omary Massare na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023. Nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kuja na Muswada huu ambao aliyetangulia ameshagusa sehemu nyingi kuonesha kwamba zipo karibu maeneo matano au sita ambayo yalitakiwa kuguswa na yeye mengi ameyapitia. Mengi yanaonekana yanaongozwa na utaratibu, teknolojia na uhalisia wa mambo ya sasa.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye eneo la nguvu za *atomic*. Tunajua kabisa Tume ya Nguvu za *Atom* inajaribu ku–*control*, kujaribu kuratibu mionzi katika mazingira yetu ya kazi. Wako watu wengi kwenye kumbukumbu nyingi utagundua wameathiriwa na mionzi na inawezekana kabisa huko nyuma uratibu haukuwa mzuri sana na ndio sababu nampongeza Mwanasheria kwa sababu ya kuja na hili. Vile vile nampongeza Waziri wa Sheria na Katiba, lakini Kamati yenyewe ambayo imeshughulika kuupitia Muswada huu na kufanya marekebisho na kuruhusu sasa uje kwetu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Bunge na Wabunge wenzangu ni kupitisha Muswada huu ukawe Sheria kwa ajili ya udhibiti wa mambo mbalimbali ambayo yanaonekana huko ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Muswada huu wa Nguvu za *Atomic, Cap* 188, Ibara ya 4, utagundua kwamba yako marekebisho yaliyofanyika hapo. Kwanza umeshughulikia marekebisho katika Kifungu cha 4 na kilichofanyika katika hilo ni kufuta Kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya. Maana yake wamebadilisha zile *levels* sasa kwenye kifungu hicho kwamba, vitu vyenye viasili vya mionzi na matumizi ya mionzi, vyenye ujazo pungufu zaidi ya *becquerel* moja kwa gramu na vinakwenda mpaka *becquerel* kumi kwa gramu. Hivi ukiangalia kwenye Muswada huu vinaonesha kabisa kwamba vitatakiwa kuwa vimeratibiwa.

Mheshimiwa Spika, huko mwanzo kama alivyosema mwenzangu viwango vilikuwa juu, sasa tumeshusha viwango hivi kuhakikisha kwamba uratibu wa vifaa vinavyotoa mionzi au vyenye uasili vya mionzi vinaenda kudhibitiwa ambavyo vimefungwa na ambavyo havijafungwa lakini kwa ujazo huu mdogo. Pia ukiangalia utabaini kwamba imeongezwa ibara ndogo ya tano kwa lengo la kupunguza vile vile uchafuzi wa mazingira yetu kwa njia hii ya mionzi. Kuna mionzi inaitwa *Alpha* na *Beta* wale waliosoma sayansi watakuwa wanaijua.

Mheshimiwa Spika, mionzi hii kwenye uso nayo imepunguza kwamba isizidi *becquerel* 0.8 kwenye uso ambao unaweza kuwa *contaminated surface*. Sasa hivi ni vitu ambavyo mwanzo vilikuwa havikudhibitiwa na kama havikudhibitiwa wapo watu wengi walikuwa wanaathirika na hili. Kwa hiyo Sheria hii inakuja kuhakikisha kwamba tunaweka sasa uratibu mzuri, watu wetu *either* wale wanaokuja na vifaa hivyo ambavyo vina mionzi hiyo au wale wanaotumia wasiweze kuathirika kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, ukienda mbele kidogo utagundua (b) kwenye ibara hiyo imeongezwa ibara ndogo ya (7) inayoonesha masharti ya ukomo wa vigezo vya msamaha kuhusu mionzi baada ya kuwa imeidhinishwa na Waziri. Ndugu yangu alisema hapa habari ya *compounding,* kwamba ni lazima tufike mahali sasa badala ya kwenda tu tunapambana kupeleka mashauri yetu kwenye mahakama. Tufike mahali fulani kuna vitu ambavyo vinaweza kufanyika nje na kama kuna msamaha unaweza

kutolewa utolewe lakini utolewe kwa ukomo gani. Hivi navyo vimeainishwa kwenye Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla marekebisho katika ibara hii yanalenga kuweka masharti ya kupunguza viwango vya msamaha kuhusu viwango vya mionzi inayotokana na mmuliko katika vitu mbalimbali ambavyo tunavitumia. Aliyetangulia alisema kuna habari ya simu, niipongeze sana Kamati, nilipongeze Bunge na nimpongeze Spika, kwa nafasi uliyotupatia kwenda pale kwenye Tume ya Mionzi, tumeona vitu vingi na tumeona kabisa watu wengi wanavyoathirika, hata *microwave* tulizonazo ambazo ni chanzo cha mionzi, ukiiacha wazi tu unaweza ukashangaa baada ya muda unafikiri unachemsha nyama kumbe unamchemsha na yule wa pembeni pale, baada ya muda utagundua ameathirika. Kwa hiyo haya mambo ni mambo muhimu na sisi tuliomba kabisa Tume ile ikiwezekana ije Bungeni hapa, ije ifundishe mambo haya ili watu wasiendelee kununua *microwave,* kununua vitu vingine na kununua simu kumbe wanaendelea kuathirika bila kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ibara ya 5 vilevile imefanyiwa marekebisho katika kifungu cha 11 utaona hapo kumeongezwa maneno kadhaa kama *dispose, learned, late* lakini vile vile *transfer, import* kwa sababu kuna watu wanaingiza vitu. Kwa hiyo yameingizwa maneno hayo kwenye Muswada huu, lengo la marekebisho haya ni kuwajumuisha wadau wote wa mionzi hii mbalimbali kupata leseni na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi wameingia kwenye matumizi ya vifaa ambavyo vinatoa mionzi ya asili au ile ambayo inaonekana inatokana tu na umulikaji lakini hawakuwa wanapata leseni, hapa kwa muswada huu sasa wanatakiwa wawe wamesajiliwa wamepata leseni. Hoja kubwa ni kufanya uratibu wa kutosha kwenye mionzi hii ambayo nimeisema. Iko mionzi ambayo ni *ionized* na mingine siyo *ionized,* lakini yote ipo katika mazingira mazuri sana kama utaitumia vibaya kwenye kuathiri. Hata Ndugu zangu wachimbaji wa madini tu huko ninakotoka mimi iko mionzi ya asili unapokwenda kule chini kama haijadhibitiwa vizuri unaweza ukashangaa ndani ya shimo lililoko mionzi ile ikakuletea athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia ukienda katika Muswada huu utagundua Kifungu katika Ibara ya 10, kulikuwa na neno limeandikwa chakula *(food stuff)*. Hii *food stuff* ndiyo walikuwa wanaenda kupima mionzi wataalam, lakini kwenye Muswada huu wamebadilisha neno *food stuff* sasa wanakwenda kwenye *food chain,* maana yake tutaanza kuipima kwanza mbegu inayoenda kupandwa na ikipimwa ile mbegu sasa tunakuja kwenye *process* mpaka kwenye chakula chenyewe.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukapanda mbegu ikiwa na mionzi, ikakua ikaenda na zao litakalokwenda kutoka mwisho likaja na mionzi. Wewe ukapima ukijua kwamba, tunachopata hapa ni *food stuff* Hapana! Tunakwenda kuanza kwenye mbegu yenyewe, kama ina mionzi izuiwe kulekule mwanzoni isipandwe. Kwa hiyo, muswada huu ni muswada wa muhimu sana kwa sababu unakwenda kuangalia afya zetu kwa ajili ya kizazi hiki na kizazi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yako mambo mengi yaliyoandikwa kwenye Muswada huu, nilitaka kugusa tu kwenye atomi hapo tuweze kujua kwamba, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba, Muswada huu unapita kwa sababu ni kawa ajili yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaabani Hanje, tutamalizia na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nami nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Kizito Joseph Mhagama ambaye ameiongoza Kamati vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alikuja na Marekebisho haya ya Sheria Mbalimbali katika Kamati yetu, kwa kweli, usikivu wake unalifanya Bunge lako kuwa na thamani na kupewa

heshima kubwa na wananchi, kwa sababu mambo ambayo tumetoka nayo juzi na sheria hii ilipokuwa inakuja hasa sehemu ya nne na ya tano ingeleta mtafaruku kidogo, Mheshimiwa *AG* amekuwa ni mtu muungwana na mstaarabu na kuona ni namna gani Bunge lako sasa litakuwa linachakata sheria kwa weledi na kwa utaratibu ambao unafaa, kesho jamii iweze kuelewa kwamba, Bunge hili liko kwa maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ambayo tunaijadili leo, tukiondoa zile ambazo *AG* ameziondoa, tunachakata sehemu tatu hasa ambazo ndiyo zinajadiliwa hapa na nitaendelea kuomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waweze kukubaliana na maelezo ya Kamati, lakini maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba, marekebisho haya ya Sheria Mbalimbali ni kwa maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, dunia inakwenda *speed* na teknolojia ambayo ipo duniani sasa ni ya nyuklia, baadhi ya nchi zetu nyingi, majirani zetu, lakini nchi ambazo zimeendelea zinaitumia nyuklia katika maeneo mbalimbali, sasa wamefika hata katika kuhifadhi vyakula kwa kutumia teknolojia hii. Kwa hiyo, tunapoenda kurekebisha sheria hii ya atomi itasaidia itasaidia Taasisi yetu ya Atom kwenda na wakati, lakini kwenda kuona namna gani ambavyo wanaisaidia nchi na wananchi wa Tanzania kuepukana na mionzi hii hatari.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inaenda kutambua watumiaji wote wa vifaa vinavyotumia mionzi. Hata mimi nilikuwa sijui kama wajenzi wa barabara wanatumia vifaa vya mionzi katika kujua uzito wa barabara, lakini baada ya kuletwa sheria hii katika Kamati na sisi kwenda kule ulikotuidhinisha kwenda katika Tume hii ya Mionzi kule Arusha, hakika kuna vitu ambavyo tumepata na kujifunza. Kama alivyosema mchangiaji aliyepita, inafaa siku moja Bunge lako lipewe semina ya kutosha juu ya masuala haya ya mionzi.

Mheshimiwa Spika, leo hii tumezungumzia kidogo, Mheshimiwa Olele-Kaita alizungumzia simu hizi, lakini Mheshimiwa Magessa amezungumzia namna gani *microwave* ilivyo hatari kwa afya ya mtumiaji na hasa anapoitumia pasipo utaratibu sahihi.

Kwa hiyo, hayo yote yanapaswa kuletwa, lakini tukapewa semina sisi kama wawakilishi wa wananchi na sisi tunaweza kuipeleka zaidi kule kwa wananchi ambao tunawawakilisha humu ndani ya jengo hili.

Mheshimiwa Spika, hata uchenjuaji wa madini kuna baadhi ya vifaa vinavyotumika vinatumia mionzi. Madini mbalimbali na hasa hizi taasisi kubwa kubwa, *mining company* kubwa kubwa ambazo zinachenjua madini, kwa hiyo semina hizi zikipatikana kwa wajumbe wako wa baraza hili kubwa la kutunga sheria kwa maana ya Bunge, itasaidia wananchi wetu kujua changamoto ambazo zinatokana na mionzi. Pia sheria hii inakuja kumpa mamlaka makubwa na mazuri Mkurugenzi wa Taasisi hii ya *TAEC*.

Mheshimiwa Spika, mwanzo kabla yake kulikuwa na leseni ambazo zinatolewa, lakini leseni zile zilikuwa zinapaswa kusainiwa na Mwenyekiti wa Bodi na aghalabu Mwenyekiti wa Bodi mara nyingi hayupo ofisini ni mtu ambaye anakuja kwa sababu ya vikao, lakini Mtendaji ambaye anafanya kazi muda wote ni Mkurugenzi Mkuu, kwa hiyo, sasa marekebisho haya yanakuja kufanya Mkurugenzi Mkuu ndiyo asaini sehemu zote ambazo watapewa watumiaji wa vifaa vyote vya aina yoyote ya mionzi ambao wanatumia vifaa hivyo, ili waweze kudhibitiwa na kuvitumia katika sura ambayo itakuwa na tija kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi amepewa mamlaka ya kufifilisha makosa. Hii inapunguza mlolongo wa kesi nyingi ambazo ziko mahakamani kwa sababu mashauri yaliyoko katika Mahakama zetu wakati mwingine yanachelewa kuamuliwa kutokana na Ushahidi, lakini mtu akikiri kosa ni rahisi sasa kufifilisha makosa na sheria hii inakuja kurahisisha mtu ambaye amekiri kosa na amelifanya kwa bahati mbaya, kwa kukusudia au bila kukusudia akaadhibiwa na ikamalizika pela na mwisho wa siku haya yanakuwa hayaendelei.

Mheshimiwa Spika, mimi ni miongoni mwa waliotembelea maabara 12 katika Taasisi hii ya Mionzi. Taasisi hii inahakikisha Watanzania wanakuwa salama na mionzi, vifaa vyote vinavyoingizwa nchini vinavyohusiana na mionzi wanavidhibiti na wanavicheki kabla havijaingia kwa watumiaji, maana yake

vinapoingizwa katika bandari zetu, katika viwanja vya ndege na maeneo mengine, wanayo changamoto pia ya watumishi ambayo watu wa Wizara ya Elimu nao watashughulika nayo, nina hakika hili nalo watalitatua.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya ya sheria tulikofika sasa kuna vifaa hivi ambavyo kwa hakika tulikuwa hatudhani kama vina madhara, hapa imezungumzwa simu na *microwave,* lakini viko vingi sana.

Mheshimiwa Spika, niishie hapa kwenye hii Tume ya Mionzi, nije kwenye Chuo cha Bandari; marekebisho haya yanakizungumzia pia Chuo cha Bandari ambacho kilikuwa kinaendeshwa kama Taasisi, kama Idara ya Serikali, ilifika mahali ilivyokuwa huko nyuma kabla ya marekebisho haya ambayo yameletwa kwako leo katika Bunge lako hili tukufu ni kwamba, Waziri ndiye anayetunga Kanuni za kuendesha chuo badala ya bodi. Kwa maana hii chuo kikiwa kama Idara ya Serikali mambo mengi yalikuwa yanakwama kutokana na utaratibu ule wa kumfikia Waziri ili aweze kutengeneza Kanuni za kuendesha chuo.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kuwashauri Wabunge wenzangu wakubaliane na marekebisho haya ya Katiba kwa sababu chuo hiki cha Bandari sasa kinaenda kujiendesha kama vyuo vingine kitaaluma, na kitafuata utaratibu na *procedure* za kawaida za uendeshaji wa vyuo vingine vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala hili la malipo ya pesa, zilikuwa zimeandikwa pesa za kigeni kabla, lakini sasa wakaja na marakebisho kwamba, zilipwe katika *terms* za *US Dollar. Terms* za *US Dollar* tumehofu kwamba tunaweza kutokana na mabadiliko yoyote, wakati wowote ikaja sarafu yoyote duniani ikapanda thamani, ikiwepo *Euro* au ikawa ndiyo inayotawala soko.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hapa hata leo asubuhi katika Bunge lako tumeona namna gani Dola imekuwa chache katika masoko ya fedha. Kwa hiyo, tumeishauri Serikali na imeridhia ofisi ya *AG* kwamba sasa badala ya kutaja tu *US Dollar* itaje fedha za kigeni, lakini chuo kiwe na *mandate* ya kuamua ni pesa gani kwa kipindi hicho inafaa kulipwa katika hiki chuo.

Mheshimiwa Spika, mengine mengi ambayo yamejadiliwa, lakini nitoe rai kwa Wabunge wenzangu kuunga mkono hoja hii na kupitisha marekebisho haya ya Sheria Mbalimbali kuwa sheria. Ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Shaabani Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Botondo, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, (Na. 2) ya Mwaka 2023. Kusema ukweli kabisa nilikuwa nimejiandaa kuchangia Sehemu ya Nne na ya Tano ya Muswada…

**SPIKA:** Kuna mtu amesimama mbele yako kwa hiyo, asogee pembeni ama aketi. Haya, endelea na mchango wako.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nilikuwa nimejiandaa kuchangia Sehemu ya Nne na ya Tano ya Muswada. Kwa kuwa, ninafahamu sana majukumu na kazi ya Bunge hili na kwa kweli imekuwa ni desturi kwamba, tunatunga sheria na tunajipa muda kwa sababu ni ukweli kwamba ukishatunga sheria unahitaji muda ili u-*practice* uone kama kuna shida ili sasa Bunge hili lirudie kazi yake ya aidha kurekebisha, kuandika upya ama kutunga sheria nyingine ambayo itakuwa kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama ambavyo ninajua kwamba, ni desturi hiyo siku zote kwenye Bunge hili tunafanya, nilitegemea pia tujadili sana kuhusiana na hili, lakini niipongeze sana Serikali kwa kuona hayo ambayo yalionekana na wengine na Kamati pia imeshauri. Kwa hiyo, nikubaliane na Kamati walivyoona kwamba, na wao wameipongeza Serikali kwa kuondoa vifungu hivi kwa sababu za sasa hivi, lakini pia niwaombe Serikali wala siyo jambo la kuwa na wasiwasi nalo, kwa sababu lengo ni kuhakikisha kwamba tunavuna rasilimali zetu kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna sheria nyingine yoyote ambayo mnafikiri kwamba, Bunge hili linahitaji lletewe ili tuireirekebishe kwa ajili ya kuvuna rasilimali za Taifa hili kwa urahisi ili Watanzania wenye rasilimali hizo wanufaike basi tusiogope kuleta. Mimi nitakuwa tayari na ninajua Waheshimiwa wenzangu pia watakuwa tayari kwa ajili ya kujadili muda wowote ambao tutaona ni wakati sahihi wa kujadili pamoja na hiki Kifungu cha Nne na cha Tano kwa sababu, tunajua kabisa kuna maslahi mapana kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu hilo sasa hivi limeshaondolewa na tutalisubiri tunajua wakati mwingine linaweza kuja, kwa sasa hivi kwenye hizi zilizobakia ninaomba nichangie Sehemu ya Tatu ya Muswada ambayo inahusiana na *Dar es Salaam Maritime Institute Act, Cap. 253,* kwa sababu, na mimi pia ni Mjumbe wa Kamati, siyo Kamati hii ni Mjumbe wa Kamati ya Elimu na hili jambo linahusiana na taasisi mojawapo ambayo inatoa elimu hiyo *specific*. Kwa hiyo, niwapongeze. Kwenye huu Muswada mzima utaona ni ukurasa wa 16 mpaka 34 umezungumza na kwa Ibara zote ambazo wameona.

Mheshimiwa Spika, nikianzia Ibara ya 17 ambayo inaainisha cheo sahihi cha Mkuu wa Chuo kuendana na *NACTE (NACTVATE),* lakini pia Ibara ya 18 ambayo imeondoa mamlaka ya Waziri kutoa ithibati kwa wanafunzi kuanzisha taasisi ya wanafunzi, tunazijua zile za *DARUSO, UDOSO* na nyingine kama hizo, lakini ya pale na kuipa Bodi. Niwapongeze sana kwa hili kwa sababu najua kwamba, Bodi wanaweza kufanya vizuri kwa *practice* ambayo tumeiona.

Mheshimiwa Spika, lakini hiyo ni (A) na (B) yake ambayo imeongeza tafsiri ya *Academic Council* ambayo ni sehemu ya marekebisho katika hizi ambazo wanazifanya kwenye hii Sheria ya Bandari. Hilo pia nilipongeze ni jambo zuri katika *practice*. Ibara ya 22 ambayo imeanzisha Baraza la Taaluma la Chuo, ninakubaliana pia na maoni ya Kamati ambayo wametoa na kwa kweli, tungekuwa na muda hata usingetosha kujadili lile jambo la mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nipongeze na kwa kweli, sisi tuko tayari kwa ajili ya kutunga hiyo sheria ili Mheshimiwa Rais akaipitishe ili mambo yaende. Na sheria hiyo nyingine ya masuala ya *atomic,* wamezungumza Waheshimiwa wenzangu na ninakubaliana na maoni yao na kwa kweli, niseme naunga mkono hoja hiyo ya kufanya marekebisho ya sheria hizi ili tuendelee ku-*practice* kazi ya Bunge hili ambayo ni kutunga sheria na kurekebisha sheria ambazo tunaona katika *practice* zinawezekana zina shida. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo. Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Katiba na Sheria, ninamshukuru sana pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Pauline Gekul, ninamshukuru sana *Attorney General* na ninamshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu kwa namna ambavyo amekuwa akiendesha vizuri Kamati hii na kutoa ushirikiano mkubwa na hasa tunapokuwa tunapitia mambo mbalimbali na hasa ya marekebisho ya Miswada mbalimbali katika Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami kwanza ninashukuru sana, nikianzia sehemu hii ya kwanza ya *Atomic Energy, Cap. 188.* Ukweli ni kwamba, jambo hili ni la muhimu na limekuja katika wakati muafaka, sote tunafahamu kwamba, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba, afya za Watanzania zinalindwa. Eneo hili limekuja katika kipindi muafaka kwa sababu litakwenda kuhakikisha kwamba, baadhi ya mambo ambayo hatukuweza kujua ama jamii kutokufahamu sasa yanaenda kusimamiwa na kuzingatiwa kiasi kwamba, afya zao zitakwenda kuwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaamini kwamba, sote tunafahamu kwamba, itawezesha sana Tume kufanya kazi zake kwa ufanisi na hivyo hata utekelezaji wa majukumu yake

unaweza ukawa unafanyika sawasawa. Pia tunaweza tukaona kwamba, kuna jambo ambalo linaenda kusaidia sana kupunguza athari za mionzi. Sote tunafahamu kwamba, mionzi imekuwa na athari kubwa, lakini tunajua katika hospitali zetu, kuna watumiaji wa vifaa mbalimbali ambao wanatumia vifaa hivi vya mionzi, lakini tumekuwa hatuwezi kudhibiti na kufuatilia kwa karibu kuona athari za mionzi hii. Kwa hiyo, sheria hii inaenda kusaidia sana kufanya ufuatiliaji na kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa sababu tunaona umuhimu wa afya za Watanzania wote kwa ujumla kwamba, ufuatiliaji na kuona hali ya udhibiti na matumizi yasiyokuwa yanafaa yanaweza kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ambacho naenda kuzungumza ni kipengele cha kifungu cha 6(a) ambacho kinalenga kuanzisha Baraza la Taaluma katika chuo chetu hiki. Kimsingi hapa unaweza ukaona katika ushauri wa Kamati kwamba, kitakuwa chini ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Chuo, lakini tusiwe na mashaka kwa sababu timu ya wataalam akiwemo Makamu wa Chuo, Wakuu wa Idara mbalimbali, Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi, Mlezi wa Wanafunzi, hawa wote ni wataalam ambao wanatosha kabisa kuifanya Bodi hii iweze kusimama vizuri na kuweza kutekeleza majukumu yake inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki ni cha muhimu sana, nami nashauri kwamba, Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwa pamoja hii inaweza ikasaidia kufanya urahisi na pengine maamuzi kwa mfano ya mabadiliko ya kubalisha vifungu mbalimbali ambavyo vinaweza vikawa vinasaidia katika uendeshaji wa vyuo, inaweza ikasaidia sana maamuzi pengine kutekelezwa kwa wakati zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia tunaweza tukaona kwamba, lengo la matumizi pia, *I mean* kuondoa hoja ya matumizi ya dola badala yake tuachie milango iwe wazi kiasi kwamba, matumizi ya fedha zozote zile zinaweza zikatumika, sote tunafahamu kwamba, malipo haya yamekuwa yakiwekewa masharti ya matumizi peke

yake ya dola. Kwa hiyo, tukipunguza tukaondoa masharti haya itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo tumeshauri kama Kamati kwamba, tuondoe neno *council* na badala yake tuweke bodi. Hii itasaidia sana, kukiwepo na bodi kama tulivyozungumza, bodi hii itakuwa imesheheni timu ya wataalam na wenye sifa mbalimbali, kwa hiyo, ufanisi ama marekebisho yoyote ya kikanuni ambayo yanaweza yakafanyika katika Bodi ama kubadilisha kanuni, yanaweza yakafanyika vizuri kwa sababu inakuwa na timu ya wataalam na wanataaluma wabobezi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali uje uhitimishe hoja yako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipatia tena fursa hii. Namshukuru pia Mwenyekiti wa Kamati na jumla ya wachangiaji ambao wamepata fursa ya kuchangia, ukimjumuisha Mwenyekiti na Wabunge wengine watano.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wa Kisekta, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Biashara, na Wizara ya Elimu. Kwa sababu, kama tunavyofahamu katika utendaji kazi wa Serikali, kila Waziri ana majukumu anayopangiwa kwa hati maalum, na kila Waziri ana wajibu wa kuhakikisha sheria tulizonazo zinakuwa hai na zinatimiza malengo yake. Kwa hiyo, nawashukuru kwa sababu wao na taasisi zao ndiyo waliibua maeneo ambayo yameonekana kwenye Muswada huu ambao ulikuwa na sehemu ambazo zimejadiliwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa ushirikiano ambao tuliupata kwa Kamati ya Bunge. Ninawiwa kulisema hili, labda niliseme kwa muktadha ufuatao: -

Mheshimiwa Spika, unatolewa wito wa kuendelea kutoa elimu zaidi katika maeneo haya. Sisi kama Serikali tunao wajibu, na Wizara zote ziko tayari kuendelea kushirikiana na Bunge kutoa elimu kwenye maeneo yote ambayo yanaibuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya haya na yanayoendelea nje, na kwa uzoefu wangu, nafikiri vile vile umefika wakati hata taratibu za Bunge nazo, itolewe elimu ili hata wananchi ambao mara nyingi wamekuwa kila mmoja anasema kwa sauti ya mwananchi, kwa niaba ya mwananchi, wajaribu kuelewa jinsi Bunge linavyofanya kazi. Kwa sababu, Serikali inapokuja na Muswada kama tulivyokuja hivi, ukaungwa mkono, maana yake kazi kubwa imefanyika ngazi ya Kamati. Kwenye Kamati sisi ambao tunawajibika kule, tumekuwa tunaona kabisa Kamati zinavyowajibika kwa wananchi waliowachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kwa mantiki hii mchakato wa Mbunge anavyopatikana kuanzia wakati wa Kura za Maoni, baadaye akachaguliwa na wananchi, baadaye asipingwe kwa utaratibu wa kisheria, akawepo humu na asiwajibishwe kwa kanuni za humu, maana yake wanahitaji pongezi na kupewa heshima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge. Ninaahidi tu kwamba, maeneo yote tuliyoyaleta, ukweli ilikuwa ni kuhuisha na kuhakikisha kwamba sheria zetu zinatimiza yale mahitaji ambayo jamii yetu na Tanzania yetu imefika leo na inakoelekea. Kwa hiyo, kama Serikali, tunaahidi kuendelea kutekeleza sheria hii ambayo sasa baada ya michango iliyotolewa, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge hili lipendezwe sasa kuingia kwenye hatua inayofuata.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 22 kina marekebisho ya Serikali na marekebisho haya ni yale ya kupunguza idadi ya Wajumbe kama ambavyo Kamati imependekeza. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sababu hii inayoanzishwa hapa ni *Academic Council*, sasa nilitaka kujiridhisha kama wale watu wa chuo wameridhia hawa *Heads of Departments of the Institute* watoke. Kwa sababu, upo uwezekano hawa *Heads* wa *institutes (Heads of Departments)*, zile *departments* zinaweza zikawa ni *Academic Departments*. Kama ni *Academic Departments*, zisipokuwa na uwakilishi kwenye *Academic Council*, nani atakayekuwa anaeleza mambo ya watu wanaotoka kwenye *departments* zao?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa marekebisho tuliyofanya, *Director of Academic Support Services* ndiye atakayefanya jukumu hilo.

**MWENYEKITI:** Unajua mimi nimetoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Director* hana uwezo wa kujua mambo yote yanayotokea kwenye *departments*. Hana uwezo huo, *unless* sisi tunasema *functions* za hii *Academic Council* ni tofauti na *Academic Council* nyingine. Kwa sababu hii ni taasisi inayotoa elimu. Kwa hiyo, zile *departments* ukiacha hawa mliosema huku chini, *Head of Legal Unit*, huyu anaweza kuwa ni kitengo cha sheria hapo. Kwa hiyo, yeye hafundishi sheria pale, lakini kinaweza kikawepo kitengo ambacho ni cha ufundishaji. Sasa, akiwa hayupo yule *Head* halafu tukamtegemea yule *Director* ndio aingie mle ndani atetee *departments* labda ziko 10, mimi sijui. Sijawahi kwenda hicho chuo, sifahamu. Nataka tu kujiridhisha kama hawa *Heads of Departments,* hizi ni *Administrative Departments* au ni *Academic Departments*?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *academics* na kwenye mjadala pamoja na taarifa kutoka kwenye taasisi husika, maelezo ya kutosheleza yalikuwa kwamba akiingia huyu *Director of Academics* mwenyewe kama anavyosomeka, halafu na huyu *Director of Academic Support Services*; huyu mmoja pia ni *for academics,* halafu yupo huyu wa *Support Services*.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Profesa Kitila ananitazama hapo. *(Kicheko)*

Maadamu ninyi mmeridhiana na Kamati, sina neno, lakini nataka tu kujiridhisha, kwa sababu, hii ni taasisi ambayo inahusika na mafunzo. Sasa hizi *departments* huenda zinahusu mafunzo. Ukisema Mkurugenzi wa Mafunzo ndio atajua, siyo rahisi. Kwa sababu, hizi *departments* huwa zianaanzisha *courses* mpya, zinaanzisha jambo fulani na lazima ziwepo kwa ajili ya wanafunzi wanaohusu mambo wanayoyasoma wao, lazima wakaseme. Sasa, kama wao hawawi sehemu na ukasema labda wataenda kama waalikwa; utaratibu wa vyuo unataka wale wanaohusika na yale mambo wawepo, wawe sehemu ya maamuzi. *(Makofi)*

Sasa wewe niridhishe tu, halafu tupitishe.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, awali utaona kwenye Muswada. Kwenye (d) kulikuwa na *Heads of Departments of the Institute* na wale wengine.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa hiyo, baada ya hoja ya uelewa kama huu kujitokeza, tukawarudishia wahusika wenyewe wakajadiliane kwa muundo wao na majukumu yao na kuja sasa na kanuni wakilishi. Kwa sababu mwanzoni ilikuwa wawakilishi 15.

Kwa hiyo, walivyowachuja na kuona kwamba uwakilishi *proper* usiokuwa na shughuli utakuwa upi, ndivyo

walivyowapunguza na kuwa tisa. Kwa hiyo, hii ndiyo *position* ambayo tunayo sasa.

**MWENYEKITI:** Sawa. Nimeelewa lakini nafikiri iko haja ya kwenda kulitazama hili jambo, hasa hili la *Academic Council*. Kwa sababu, hata *Dean of Students* naona hapa mmesema kwamba aondolewe. Kule wanajadili matokeo ya wanafunzi. Mwanafunzi alikuwa na shida fulani, wanapaswa kufanya maamuzi juu ya yule mwanafunzi, nani anayejua taabu za huyo mwanafunzi? Mimi sijui! *(Makofi)*

Mimi nimetoka huko kwenye vyuo, najua wanafunzi huwa wana mambo mengi. Hapa pia ameondolewa. Huyu *Internal Audit Unit*, ni sawa, lakini ameondolewa *Head of Quality Management Unit*. Sasa hawa watu wanashauriwa na nani mambo ya *quality of the education that they are giving to these students? (Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) ambacho hakijaguswa, Baraza linaweza ku-*co-opt*. Ndiyo maelezo ambayo tulikuwa tunasema kwamba endapo uwakilishi ambao sasa umewekwa baada ya yale marekebisho yaliyopo kwenye jedwali, Baraza limekaa na kukawa na mahitaji. Inabaki *leeway* kwenye *sub-section three*. *"The Council may co-opt any person to attend and deliberate on specific matters as the Council may determine but such person shall not have the right to vote." (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa jamani. Nafikiri kwa sababu Kamati yetu imependekeza jambo hili kwamba watu wapungue idadi na Serikali imeridhia, tutaenda na mawazo hayo, lakini nafikiri hoja ya msingi iko pale pale. Hii ni taasisi inayotoa elimu. Wale watoa elimu lazima wawe Wajumbe wa *anything you call academic*. Ingekuwa ni ya utawala kama ile Bodi nyingine, kweli utasema siyo lazima wawepo, lakini unazungumia elimu wanayopewa hawa wanafunzi, halafu wale watoa elimu wasiwe sehemu. Kidogo inaleta changamoto, kwamba huyu Mkurugenzi atajua habari za kwenye *departments* ambazo ni *Academic Departments*. Siyo rahisi. *(Makofi)*

Maadamu tumefika ngazi hii kwa sasa, hatuwezi kurudi nyuma, lakini hoja ya msingi ni *academic departments* watazame vyuo vingine. Nataka kuamini walikuwa wametazama vyuo vingine walivyoleta kwamba *Heads* wawe *members*. Sawa. Uzuri, Bunge ndiyo kazi yetu kutunga sheria jamani. Wao wakalitazame halafu wataona, kama kuna sababu, watatuletea tena. Ndiyo kazi yetu. Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi. Sasa tunawarejeshea wao ili sisi tufanye kazi yetu ya kutunga sheria, wao wakalitazame jambo hili, hii *Academic Council,* watu gani wawe wanaingia huko?

Hicho ni kifungu cha 22 ambacho tulikuwa tunakizungumzia. Kwa haya yaliyosemwa hapa, tutaenda nayo kwa sura hii iliyopo kwa sababu haina athari ya moja kwa moja, lakini wataenda kutazama, kama kuna sababu ya kuwaongeza hawa ambao ni *Heads of Departments* ambazo ni *Academic Departments,* wataleta marekebisho, halafu tutaifanyia kazi tena hii sheria.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne inafutwa na Serikali.

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Sehemu ya Nne inafutwa ambayo inahusu mabadiliko kwenye sheria yetu ile ye *Amendment of the Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act*. Mapendekezo yaliyokuwa yameletwa yanafutwa yote.

Waheshimiwa Wabunge, tunaafiki kufuta marekebisho haya yaliyopendekezwa?

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano inafutwa na Serikali.

Kifungu cha 37
Kifungu cha 38

**MWENYEKITI:** Sehemu ya Tano inahusu *Amendment of the Natural Wealth and Resources Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms Act, CAP 450*, nayo inafutwa kwa maana ya kwamba Bunge halijapitisha marekebisho haya, ikiwa Wabunge mnaafiki.

Waheshimiwa Wabunge, kufutwa kwa sehemu hii ambayo ilikuwa inapendekeza marekebisho mnakubali?

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita inakuwa Sehemu ya Nne.

**MWENYEKITI:** Haya, kwa maana ya namba Sehemu ya Sita inakuwa ya Nne, sasa tunaendelea.

Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kufutwa kwa Sehemu ya Nne na ya Tano, Serikali imefanya mpangilio wa vifungu kwa maana ya *renumbering*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mpangilio na namba ya vifungu na mabadiliko yake ambayo yanatokana na kufuta ile Sehemu ya Nne na Tano, tunakubaliana nayo?

*(Mabadiliko ya mpangilio wa namba za vifungu kutokana na kufuta Sehemu ya Nne na ya Tano yalikubaliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2023),* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2023),* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji kuhusu hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2023)*.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki. Sasa tunaendelea na utaratibu wetu wa kutunga sheria. Katibu. *(Makofi)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Tatu, kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamejitokeza wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria Hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in the Implementation)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2023 (The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2023) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa Mara ya Tatu. Kwa utaratibu tuliojiwekea, tumekamilisha utungaji wa sheria, kwa maana ya kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali zilizokuwa zimeletwa kwetu. Kwa hiyo, Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2023)*, umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu, ili Mheshimiwa Rais naye aweze kufanya yale ambayo Katiba yetu inataka naye awe ameshiriki katika hili zoezi zima, tutampelekea ili aweze kusaini Muswada huu kama ataona inafaa, halafu tutawaletea taarifa kama ilivyo ada.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa ushiriki wenu katika kuyapitia marekebisho haya ambayo baadhi yenu mmepata nafasi ya kuchangia. Natumia fursa hii kuipongeza sana Kamati yetu ya Utawala, Katika na Sheria, wamefanya kazi nzuri sana na wameweza kulisaidia Bunge kufanya maamuzi haya ambayo tumeyafanya siku ya leo. Mapendekezo mengi ambayo walikuwa wameyatoa kama Kamati, yamepokelewa na upande wa Serikali wameyafanyia kazi na mengi wameyakubali, wamefanya marekebisho hapa na pale. Kwa hiyo, natumia pia fursa hii kuishukuru Serikali kwa ushirikiano mzuri katika zoezi la utungaji sheria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo, nawashukuru pia Wabunge wote kwa ushiriki wenu katika hili zoezi zima la utungaji wa sheria, kwa sababu lazima sote tuwepo hapa ili tuweze kufanya hii kazi. Kwa hiyo, nawashukuru wote mlioshiriki pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na marekebisho yote ambayo yamefanywa katika Muswada huu, nalazimika kusema eneo moja maana limekuwa likisemwa huko nje na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wale ambao baadhi yao walikuja kwenye Kamati na wengine walitoa maoni yao kwenye Kamati kwa njia ya maandishi. Kwa hiyo, wafahamu tu kwamba maoni yao yamefanyiwa kazi kwa sehemu kubwa.

Pia yale maeneo ambayo yalikuwa yakizungumzwa sana huko nje kuhusu mabadiliko ambayo yaliwekwa kwenye Sehemu ya Nne na Tano kwenye Muswada ule wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, kwa maana ya Mabadiliko yaliyokuwa yanapendekezwa kwenye Sheria yetu ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, Cap. No. 449* na marekebisho ambayo yalikuwa yanapendekezwa kwenye sheria yetu ya *The Natural Wealth and Resources (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, Cap. No. 450*, Bunge halijayakubali. Kwa hiyo, hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika katika sheria hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ni muhimu niseme hilo, kwa sababu pamoja na marekebisho mengine, limezungumzwa

sana na wadau huko nje. Kwa hiyo, Bunge limefanyia kazi maoni yao na Serikali imekubaliana na Bunge katika zoezi hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, natumia pia fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali, ambao huwa wakipata wito wa Bunge kuja kutoa maoni yao, wanajitokeza kwa kadri wawezavyo. Nyakati nyingine tunakuwa na changamoto ya muda, lakini bado wanajitahidi kweli kutoa maoni yao. Wengine wanakuja mpaka mbele ya Kamati na wengine wanatoa maoni yao kwa maandishi. Natumia fursa hii kuwashukuru sana wote wanaotoa maoni katika kulisaidia Bunge letu liweze kufanya maamuzi yale ambayo yanapaswa kufanywa. Pia, ni vizuri tukifanya maamuzi wakati ushauri wa wananchi tumeshausikia. Kwa hiyo, tunawashukuru kwa kushirikiana na Bunge katika zoezi hilo la kutunga sheria na wakati mwingine katika mambo mengine pia ambayo huwa tunawaomba ushauri. Ahsanteni sana wote kwa kushiriki zoezi hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, anawatangazia Wabunge wote ambao wanatoka maeneo wanayolima tumbaku au mikoa inayozalisha tumbaku kwamba wakutane Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge siku ya leo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaotoka mikoa inayolima tumbaku mnaalikwa Ukumbi wa Msekwa mkaonane na Mheshimiwa Waziri huko.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ratiba tuliyokuwa tumeipanga kwa siku ya leo tumeshahitimisha. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.06 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 30 Agosti, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*